**RIPOTI YA KAMATI YA BAJETI**
**YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**
**KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018**

## SEHEMU YA KWANZA

## UTANGULIZI

Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi ni miongoni mwa Kamati nane (8) za Kudumu za Baraza iliyoundwa chini ya Kanuni ya 106 ya Kanuni za Baraza, Toleo la mwaka 2016. Aidha, Majukumu yake yametajwa katika Jadweli la kwanza la Kanuni hizo.

Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi imeundwa kwa lengo la kuliwezesha Baraza la Wawakilishi kupata fursa pana zaidi ya kuchambua, kushauri na kufuatilia kwa kina mchakato mzima wa Bajeti ya Serikali, na hatimae kuishauri Serikali ipasavyo. Kimsingi kabla ya kuanzishwa kwa Kamati ya Bajeti, majukumu ya Kamati hii yalikuwa yakitekelezwa na Kamati ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza. Hata hivyo, Kamati ya Wenyeviti haikuwa na fursa pana ya kusimamia Bajeti ya Serikali pamoja na kuishauri Serikali katika mchakato mzima wa Bajeti kutokana na uchache wa muda ambao uliotengewa kwa ajili ya kazi hiyo.
Kwa kuwa Wajumbe wa Kamati ya Wenyeviti walikuwa ni Wajumbe wa Kamati nyengine za kisekta, wasingeweza kutekeleza majukumu ya Kamati mbili za kisekta kikamilifu kwa wakati mmoja.

## MAJUKUMU YA KAMATI YA BAJETI YA BARAZA LA WAWAKILISHI

i. Kujadili na kutoa maoni na ushauri kuhusu uandaaji wa mwongozo wa kutayarisha Mpango na Bajeti ya Serikali kwa kila mwaka;
ii. Kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali;
iii. Kufanya utafiti na uchambuzi kuhusu sera za kodi, sera za fedha, na sera za kiuhasibu zilizopendekezwa na Serikali;
iv. Kujadili na kutoa maoni na ushauri kuhusu vyanzo vya mapato ya Serikali, na mapendekezo ya hatua za kupunguza utegemezi wa kibajeti;
v. Kutoa Ushauri wa jumla kuhusu bajeti ya Serikali kwa Baraza na Kamati za Kudumu za Baraza;
vi. Kuchambua na kutoa maoni na ushauri kuhusu Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaopendekezwa na Serikali;
vii. Kuchambua hoja zitakazojitokeza kwenye Kamati za Kudumu za Baraza wakati wa kujadili Bajeti za Wizara kwa ajili ya kuishauri Serikali;

viii. Kuchambua Mapendekezo ya jumla ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na matumizi;

ix. Kufikiria na Kuchunguza Mswada wa Makadirio na Mapato ya matumizi ya mwaka;

x. Kuchambua mapendekezo ya Serikali endapo itataka kuwasilisha katika Baraza Mswada wa Matumizi ya Nyongeza kwa mujibu wa Kanuni ya 101 ya Kanuni za Baraza;

xi. Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwenye Ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia na kutathmini taarifa ya Wizara juu ya utekelezaji wa maagizo hayo na kuwasilisha Barazani maoni ya Kamati kuhusu taarifa hiyo.

## WAJUMBE WA KAMATI

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Mohamed Said Mohamed | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Bahati Khamis Kombo | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Shehe Hamad Mattar | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Zulfa Mmaka Omar | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Abdalla Ali Kombo | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Asha Abdalla Mussa | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Simai Mohammed Said | Mjumbe |
| 8. | Ndg. Abdalla Ali Shauri | Katibu |
| 9. | Ndg. Asha Said Mohamed | Katibu |
| 10. | Ndg. Kassim Tafana Kassim | Katibu |

## SEHEMU YA PILI

## UTEKELEZAJI WA KAZI ZA KAMATI

Kwa mwaka wa Fedha 2017/2018 Kamati ya Bajeti imefanya kazi mizunguko mitatu, Mzunguko wa kwanza ulianzia tarehe 28/08/2017 hadi tarehe 8/09/2017 ambapo Kamati ilifanya kazi Unguja na katika Mzunguko wa pili ulioanzia tarehe 13/11/2017 hadi tarehe 24/11/2017 Kamati ilifanya kazi Unguja na Dar es Salaam. Aidha, katika Mzunguko wa tatu Kamati ilifanya kazi Pemba na Unguja kuanzia tarehe 15/01/2018 hadi tarehe 26/01/2018.

Katika kutekeleza Majukumu yake, Kamati ilikutana na Wizara na Taasisi mbali mbali za Serikali, Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza na kujadiliana kuhusu mchakato wa Bajeti ya Serikali na Mipango ya Maendeleo. Aidha, kwa kuzingatia umuhimu wa wadau Kamati ilikutana na wadau mbali mbali kutoka taasisi binafsi, wataalamu pamoja na Wawakilishi wa Taasisi za Serikali kwa lengo la kubadilishana uzoefu na Kamati kuhusu masuala mbali mbali yanayohusu Uchumi, Biashara, Sera za Kodi, Utalii, na Uwekezaji. Vikao hivyo vililenga kuisadia Serikali katika kuimarisha usimamizi na utekelezaji bora wa Bajeti na Mipango ya

Maendeleo sambamba na kubuni njia za kuimarisha mapato kwa kuongeza ufanisi pamoja na kuibua vyanzo vipya vya ukusanyaji mapato.

## MAENEO YALIYOFANYIWA KAZI NA KAMATI YA BAJETI

1. Kupitia taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa robo ya nne ya mwaka 2016/2017, robo ya kwanza na robo ya pili ya mwaka 2017/2018;
2. Benki kuu ya Tanzania Tawi la Zanzibar;
3. Mfuko wa Hifadhi ya Jamii;
4. Mamlaka ya Uwekezaji na Ukuzaji wa Vitega Uchumi (ZIPA)
5. Kutembelea Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi EPZA –Dar es Salaam;
6. Mamlaka ya Mapato TRA – Dar es Salaam;
7. Wizara ya Fedha na Mipango –Dar es Salaam;
8. Tume ya Pamoja ya Fedha JFC –Dar es Salaam.
9. Shirika la Biashara la Taifa – ZSTC;
10. Kiwanda cha Makonyo;
11. Hospitali ya Abdulla Mzee – Mkoani;
12. Ujenzi wa Skuli za Sekondari za kisasa kwa upande wa Pemba;
13. Wizara ya Kilimo, Maliasili na Mifugo;
14. Mradi wa Ujenzi wa Jengo Jipya la Abiria la Uwanja wa Ndege " Terminal II" ;
15. Idara ya Serikali Mtandao E-government;
16. Mradi wa Bandari ya Mpiga Duri- Maruhubi;
17. Ukanda wa Shughuli za Mafuta na Gesi- Mangapwani;
18. Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu – Fumba;
19. Mradi wa Ujenzi wa Kiwanja cha Mao dze Tong;

## TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI ROBO YA NNE

## (APRILI – JUNI 2016/2017)

Kamati ya Bajeti katika kutekeleza majukumu yake ilipokea taarifa mbali mbali ikiwa ni pamoja na taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha Aprili – Juni 2016/2017. Kamati ilipokea taarifa ya mapato kwa kipindi cha miezi mitatu (Aprili - Juni) ya Bajeti ya mwaka 2016/17. Katika mwaka wa fedha wa 2016/2017, Serikali ilikadiria kukusanya jumla ya TZS 841.5 bilioni ikijumuisha TZS 482.4 bilioni kutoka vyanzo vya ndani, TZS 326.1 Bilioni kutoka washirika wa maendeleo na TZS 33 bilioni ikiwa ni mikopo ya ndani, ambapo kwa kipindi cha miezi mitatu (Aprili – Juni ) jumla ya TZS 142.15 bilioni zilikusanywa, ikijumuisha makusanyo ya ndani yaliyofikia TZS 132.08 bilioni  na mapato kutoka nje yaliyofikia TZS 10.06 bilioni. Kiujumla mapato yaliyoanishwa yote yanatokana na mapato ya kodi kutoka ZRB, TRA na makusanyo ya Kodi ya mapato inayotokana na wafanyakazi wa  Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania waliopo Zanzibar (PAYE), mapato ya mawizara na mapato yanayotokana na vianzio vyengine ikiwemo washirika wa maendeleo na mikopo.

Kwa upande wa matumizi, kwa kipindi cha Aprili – Juni matumizi halisi yalifikiwa jumla ya TZS 171.10 bilioni, matumizi hayo yalijumuisha mishahara TZS 68.38 bilioni, Matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali ya TZS 44.05 bilioni, Ruzuku kwa Taasisi TZS 12.52 bilioni na matumizi mengineyo ya Kuendesha Ofisi TZS 19.85 bilioni.

## TATHMINI YA KAMATI JUU YA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI ROBO YA NNE (APRIL – JUNI 2016/2017)

Kamati ilichambua na kutathmini taarifa ya Bajeti kwa kipindi cha Aprili – Juni 2016/2017 na kubaini yafuatayo:-

1. Mapato yanayokusanywa na Serikali hayaendi sambamba na matumizi yanayofanyika kwa vile mapato yanayokusanywa ni madogo ukilinganisha na matumizi yenyewe. Kwa kipindi cha Aprili – Juni mapato yaliyokusanywa yalifikia jumla ya TZS 142.15 bilioni na matumizi yaliyofanyika kwa kipindi hicho yalifikia jumla ya TZS 171.10 bilioni ambapo matumizi hayo yalijumuisha mishahara TZS 68.38 bilioni, Matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali ya TZS 44.05 bilioni, Ruzuku kwa Taasisi TZS 12.52 bilioni na matumizi mengineyo ya kuendesha ofisi TZS 19.85 bilioni.

2. Kwa kipindi cha Aprili – Juni matumizi yaliyofanyika yanayotokana na fedha za washirika wa Maendeleo ni asilimia 53%. Hali inayoonesha kuwa, kuna changamoto ya upatikanaji wa fedha zilizopangwa kupokelewa kutoka kwa washirika hao na kupelekea kuathiri utekelezaji wa shughuli za miradi mikubwa iliyopangwa kwa kipindi husika.

3. Serikali katika kutekeleza majukumu yake inategemea pia mapato yanayotokana na misaada ya kibajeti. Kwa vile misaada hii upatikanaji wake unategemea na kuingiziwa

kwa misaada hiyo kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hivyo kuchelewa kupatikana kwa misaada hiyo kwa Serikali hiyo kunakwaza utekelezaji wa shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

4. Kamati imebaini kuwa licha ya Serikali kufikia lengo la ukusanyaji wa mapato kwa taasisi zake mbali mbali, bado matumizi yanayofanyika kutokana na mapato hayo hayajaweza kufikia kiwango cha kupatikana kwa huduma bora nchini. Bado kuna kuzorota kwa baadhi ya huduma katika sekta mbali mbali kama vile miundombinu ya barabara na suala la usimamizi na ustawi wa miji yetu.

5. Aidha, Kamati imeweza kuona kuwa Serikali bado mapato yake mengi yanategemea kutoka katika vyanzo vya kodi, licha ya kuwepo kwa vyanzo vyengine kama vile mapato kutoka washirika wa Maendeleo bado vyanzo hivyo havijawa vya uhakika wa kuiingizia mapato Serikali kwa vile kuna ucheleweshaji katika upatikanaji wa fedha zake.

6. Kamati imeweza kubaini kuwa matumizi makubwa ambayo yanayofanywa na Serikali yanajielekeza zaidi katika utekelezaji wa shughuli za kawaida kuliko shughuli za maendeleo. Katika kipindi cha Aprili – Juni, jumla ya matumzi ya kawaida yalifikia asilimia 107, na matumizi ya maendeleo yalifikia asilima 53.

7. Kamati imebaini umuhimu mkubwa wa kuwepo kwa kodi ya miundombinu kwa vile ukusanyaji wa kodi hiyo unaridhisha. Kwa kipindi cha miezi mitatu kodi iliyokusanywa ilifikia Jumla ya TZS 6.18 bilioni sawa na asilimia 98 la lengo.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Kwa kuwa mapato yanayokusanywa na Serikali ni madogo ukilinganisha na matumizi, Kamati inaishauri Serikali kueka vipaumbele katika matumizi yake ili kuweza kuwa na bajeti yenye uhalisia na yenye kutekelezeka.

2. Kwa kuwa Serikali inafanya matumzi makubwa zaidi katika utekelezaji wa kazi za kawaida, Kamati inaishauri Serikali wakati wa kufanya matumizi yanayohusiana na miradi ya maendeleo, kuweka kipaumbele zaidi katika uwekezaji wa miradi yenye ufanisi na tija kwa jamii. Kufanya hivyo kutapelekea kutoa fursa kwa wananchi walio wengi katika kupata ajira, kujiongezea kipato, maarifa na ujuzi kutokana na miradi hiyo.

3. Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango Zanzibar kupanga mikakati madhubuti ya kufuatilia fedha za misaada ya kibajeti kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano licha ya kuwepo na changamoto ya kuchelewa katika kupatikana kwake, ili ziweze kusaidia utekelezaji wa shughuli za kibajeti.

4. Kwa kuwa Serikali imekuwa na vyanzo vya mapato vinavyotokana na kodi ikiwemo kodi ya miundombinu, Kamati inaishauri Serikali kupitia kodi hizo zinazokusanywa

kuimarisha maeneo ya miundombinu na usafirishaji kwani katika sehemu hizo watumiaji wake wengi ndio walipaji wa kodi hizo.

5. Katika suala zima la ukusanyaji wa kodi, Kamati inazitaka taasisi zinazohusika na ukusanyaji wa kodi (ZRB) kuweka misingi madhubuti na ya usawa katika kukusanya kodi na kutoa huduma kwa usawa kwa wananchi ili hatimae kodi iweze kupatikana kwa ufanisi zaidi.

## TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI ROBO YA KWANZA (JULAI - SEPTEMBA 2017/2018)

Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Robo ya Kwanza mnamo tarehe 14/12/2017. Taarifa hiyo ilijumuisha mapato, matumizi, utekelezaji wa mpango wa maendeleo na mwenendo wa uchumi wa Zanzibar.

Kamati iliarifiwa kuwa kwa mwaka wa Fedha wa 2017/2018, Serikali imepanga kukusanya jumla ya TZS 1,087.4 bilioni, zikihusisha mapato ya ndani ya TZS 675.9 bilioni, mapato kutoka nje TZS 381.5 bilioni na TZS 30 bilioni mikopo ya ndani. Katika mapato hayo TZS 590.8 zitahusisha kazi za kawaida na TZS 496.6 bilioni ni kwa utekelezaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo.

Kwa kipindi cha Julai – Septemba 2017/18, Serikali haikuweza kupata gawio la faida kutoka kwenye mashirika kutokana na kutokufungwa kwa mahesabu ya mashirika hayo na kutokufanyika kwa ukaguzi wa mahesabu. Aidha Serikali pia haikupata Gawio kutoka Benki kuu

Ukuaji wa Deni la Taifa lililofikia Jumla ya TZS 401.6 bilioni ambapo deni la ndani ni TZS 124.8 bilioni na deni la nje ni TZS 276.8 bilioni. Ukuaji wa deni hilo kunachangiwa na kuongezeka kwa malipo ya kiinua mgongo kwa wastaafu wa Serikali na kuhusiana na deni la nje ni kutokana na mabadiliko ya thamani ya shilingi dhidi ya dola za kimarekani uliosababishwa na hatua zilizochukuliwa na Benki Kuu ya Marekani ya kupandisha riba yake.

Kamati pia ilipokea taarifa inayohusiana na mwenendo wa uchumi wa Zanzibar kwa kipindi cha nusu mwaka (Januari – June 2017). Taarifa hii haikwenda sambamba na taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha Julai – Septemba, kwa vile imetofautiana muda wa uwasilishwaji wake. Hivyo uwasilishaji na uchambuzi wa taarifa ya mwenendo wa Uchumi wa Zanzibar ulikuwa kwa kipindi cha nusu mwaka (Januari – Juni 2017).

### Ukuaji wa Pato la Taifa

Kwa kipindi cha Januari – Juni 2017, Kamati iliarifiwa kuwa, uchumi umekuwa kwa kasi ya asilimia 6.3 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimai 5.2 kwa mwaka 2016. Ukuaji huo umetokana na kuimarika zaidi kwa Sekta ya huduma na kuongezeka kwa idadi ya watalii wanaoingia nchini.

**Mfumuko wa Bei**

Kamati ilipokea taarifa kuwa, kwa kipindi cha Januari – Juni 2017, kasi ya mfumuko wa bei za bidhaa nchini imefikia wastani wa asilimia 5.8 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 6.2 kwa kipindi kama hicho cha mwaka 2016. Sababu iliyopelekea kushuka kwa kasi ya mfumuko wa bei ni kushuka kwa bei ya bidhaa muhimu kama vile mchele, sukari, ndizi, samaki na nishati za mafuta, na pia kushuka kwa bei za vyakula katika soko la dunia kumepelekea utulivu wa bei.

**Mwenendo wa Utalii**

Sekta ya utalii ni sekta inayotegemewa katika kukuza uchumi wa Zanzibar. Kamati imebaini ongezeko la watalii kwa kipindi cha Januari – Juni 2017 ambapo watalii walioingia nchini walifikia 170,581 ukilinganisha na watalii 143,851 waliongia mwaka 2016.

Licha la ongezeko kubwa la uingiaji wa watalii nchini, Kamati imebaini kuwa sekta hii bado ina changamoto katika utekelezaji wa majukumu yake kwa vile mapato yanayotokana na utalii bado hayajatumika ipasavyo katika kurekebisha kasoro mbali mbali zilizopo katika sekta hiyo na hatimae kuimarika kwa sekta hii kiujumla. Aidha bado kuna changamoto ya utaalamu wa kuiendesha na kuisimamia sekta hii, pamoja na bageti ndogo inayotengwa katika kuutangaza utalii kimataifa ambayo haiendani na uhalisia wa mahitaji ya soko la utalii.

**Uagiziaji na Usafirishaji Bidhaa**

Kamati iliarifiwa kuwa Thamani ya usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi imeongezeka na kufikia TZS 64.9 bilioni katika kipindi cha Januari – Juni 2017 ikilinganishwa na TZS 46 bilioni kwa mwaka wa 2016. Ongezeko hilo limetokana na usafirishaji wa zao la karafuu. Aidha uagiziaji wa bidhaa kutoka nje umeongezeka na kufikia TZS 188.7 bilioni katika kipindi cha Januari – Juni 2017, ikilinganishwa na TZS 143.2 bilioni kwa kipindi cha 2016. Kuongezeka kwa uagiziaji huo ni kutokana na mahitaji ya bidhaa za mashine, vifaa vya umeme, vyombo vya moto na vipuri vyake.

**Uekezaji Binafsi kupitia Mamlaka ya Uekezaji na Ukuzaji wa Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA)**

Kamati ilipokea taarifa inayohusiana na uekezaji Binafsi kupitia ZIPA na kubaini kuwa, kwa kipindi cha Januari – Juni 2017 miradi imefikia 11 yenye thamani ya Dola za Kimarekani USD 186.4 milioni ikilinganishwa na miradi 6 yenye thamani ya Dola za Kimarekani USD 29.3 milioni kwa kipindi cha 2016 sawa na ongezeko la asilimia 83 kwa idadi ya miradi.

## TATHMINI YA KAMATI JUU YA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI ROBO YA KWANZA (JULAI – SEPTEMBA 2017/2018)

1. Kwa kipindi cha Julai – Septemba 2017, Serikali imekusanya jumla ya TZS 160.5 bilioni kutoka vyanzo vya ndani vya mapato, sawa na asilimia 101 ya makadirio ya kukusanya

TZS 158.9 bilioni. Kwa ujumla Kamati imeweza kuona kuwa ukusanyaji wa mapato umefikia malengo, ingawaje kumekuwepo na matumizi makubwa zaidi kuliko uwezo wa Serikali.

2. Kwa kipindi cha Julai – Septemba 2017/18 , Kamati imeweza kubaini kuwa utekelezaji wa shughuli za miradi ulijikita zaidi katika miradi ya kijamii ikiwemo mradi wa huduma za jamii (ZUSP), Programu ya kudhibiti malaria, Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Msingi na Mradi wa Maji. Kiujumla miradi ya aina hii inasaidia katika kukuza ustawi wa jamii na sio kuongeza mapato ya Serikali.

3. Kwa upande wa matumizi, kwa robo hii Serikali ilikadiria kutumia jumla ya TZS 184.8 bilioni ikiwa TZS 155.8 bilioni ni kwa utekelezaji wa kazi za kawaida sawa na asilimia 84.3% na TZS 28.9 bilioni ni kwa matumizi ya shughuli za maendeleo sawa na asilimia 15.6%. Kamati imebaini kuwa, bado matumizi kwa utekelezaji wa kazi za kawaida ni makubwa ukilinganisha na matumizi ya shughuli za maendeleo kutokana na utegemezi mkubwa wa Bajeti ya Serika kutoka kwa washirika wa maendeleo.

4. Kamati imeweza kufahamu kuwa, miongoni mwa vipaumbele vya Serikali kwa mwaka wa 2017/18 ni kuimarisha miundombinu ya maeneo ya uingiaji nchini yanayojumuisha bandari na viwanja vya ndege. Hata hivyo, licha ya kuwepo kwa vipaumbele hivyo, Kamati imebaini kuwa mradi wa ujenzi wa jengo la uwanja wa ndege (terminal II) utekelezaji wake si wa kuridhisha kutokana na muda pamoja na gharama kubwa iliyotumika.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**1.** Kwa kuwa matumizi ya Serikali ni makubwa ukilinganisha na mapato yanayopatikana, Kamati inaishauri Serikali kuweka vipaumbele katika kufanya matumizi ili yawe yenye uhalisia na yenye kuleta tija kwa jamii.

2. Kamati inaishauri Serikali iweke mikakati madhubuti juu ya ufuatiliaji na upatikanaji wa gawio kutoka kwa mashirika na Benki Kuu, ili fedha inayopatikana itumike kwa maendeleo ya nchi.

3. Pamoja na juhudi za Serikali za kuendeleza miradi mbali mbali ya kijamii nchini, Kamati inaishauri Serikali kuelekeza nguvu zake katika uekezaji wa miradi ya maendeleo yenye kujihusisha na uzalishaji wa bidhaa kwa lengo la kutoa ajira, ujuzi na bidhaa na kuongezea upatikanaji wa bidhaa nchini sambamba na kupunguza uagiziaji wa bidhaa ambao unaigharimu nchi kwa kutumia fedha nyingi za kigeni.

4. Kuhusiana na Deni la Taifa ambalo linaendelea kukuwa siku hadi siku, Kamati inaishauri Serikali kuchukua jitihada za makusudi za kupunguza kasi ya ukuaji wa deni hilo ikiwa ni pamoja na kupunguza utegemezi wa Bajeti yake kwa kukopa nje

ya nchi (washirika wa maendeleo) na badala yake bajeti itegemee zaidi rasilimali fedha zilizopo nchini.

5. Kwa kuwa Serikali ina miradi mingi ya maendeleo ambayo utekelezaji wake umekuwa wakusuasua kutokana na kutopatikana fedha, Kamati inashauri katika utekelezaji wa miradi hiyo, kuwepo na vipaumbele kwa kutekeleza miradi michache yenye kutekelezeka na yenye kuleta tija kwa jamii.

6. Kuhusiana na mwenendo wa uchumi wa Zanzibar, Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango kuangalia kwa karibu viashiria vya uchumi kama vile Pato la Taifa (GDP), mfumuko wa bei, mwenendo wa biashara (mauzo ya ndani na ya nje), ukuaji wa Deni la Taifa na ukuaji katika sekta mbali mbali za uchumi. Kwa kuwa viashiria hivyo ndivyo vinavyotao sura halisi ya ukuaji wa uchumi, na kuyumba kwa viashiria hivyo kuna athari kubwa katika maendeleo ya jamii hasa katika kupunguza mapato ya Serikali na hivyo kuongeza nakisi ya Bajeti na hatimae kushindwa kutekeleza vipaumbele vya Miradi ya maendeleo.

## TATHMINI YA KAMATI JUU YA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI ROBO YA PILI (OKTOBA – DISEMBA 2017/2018)

### Deni la Taifa

Hadi kufikia Disemba 2017/2018 Deni la taifa limeongezeka kwa asilimia 15, ingawaje bado linaonekana kuwa himilivu, hata hivyo iwapo kasi ya ongezeko la itaendelea kwa kiwango kubwa itailazimu Serikali kutumia fedha nyingi kuligharamia na inaweza kuathiri bajeti ya Serikali.

### Mpango wa Maendeleo

Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Mpango wa Maendeleo unalenga kutekeleza jumla ya Programu 27 (program mbili ni mpya) na miradi 46 (miradi 11 ni mipya) ya Maendeleo. Kamati inapata hofu juu ya kupanga kutekeleza miradi mingi katika mwaka mmoja hasa kwa kuzingatia kuwa, upatikananji wa fedha za Maendeleo umekuwa wa kusuasua sana.

### Mapato

Kwa kipindi cha (Oktoba - Disemba 2017/2018) Serikali imekusanya Tsh 182.29 bilioni sawa na asilimia 93.73 ya Malengo. Kutofikia malengo ya makusanyo hayo ni kutokana na kushuka mapato ya ndani, ambapo Serikali ilikusanya Tsh 159.82 kati ya Tsh 173.99 za makadirio. Aidha, Mapato ya vyanzo vya nje yameweza kuvuka malengo kwa kufikia asilimia 109 ya Makadirio. Hata hivyo, ni vyema mkazo zaidi ukawekwa katika kukusanya mapato ya ndani kwa kuwa mapato ya nje kawaida hayana uhakika katika upatikanaji wake.

**Matumizi**

Kwa robo ya pili ya mwaka 2017/18, Serikali ilikadiria kutumia jumla ya TZS 252.27 bilioni na matumizi halisi yaliyofanyika ni TZS 204.18 bilioni sawa na asilimia 80.9 ya makisio ya jumla. Matumizi haya ni makubwa ukilinganisha na mapato yaliyokusanywa ya TZS 182.29 bilioni.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Kutokana na umuhimu wa Sekta ya Kilimo kwa uchumi wa nchi, Kamati inashauri Serikali iongeze juhudi za kuimarisha sekta hiyo kwa kuendeleza miradi ya umwagiliaji, kuwapatia mafunzo wakulima juu ya namna ya kulima kilimo cha kisasa, kuwatafutia masoko pamoja na kuimarisha viwanda vidodo vidogo kwa ajili ya kusarifu mazao, sambamba na kukitumia kisiwa na Pemba ambacho kina rutba ya kutosha katika kuendeleza kilimo cha kisasa cha mboga mboga.

2. Kamati inasisitiza Serikali kuwa waangalifu sana katika Utekelezaji wa Miradi mikubwa ya kitaifa ambayo kimsingi huigharimu Serikali fedha nyingi na inaathiri Bajeti ya nchi kwa kiasi kikubwa hususan pale ambapo malengo ya miradi hiyo haitofikiwa. Aidha, Kamati inashauri Wizara ya Fedha na Mipango kupitia kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini, kushirikiana na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ili kupata utaalamu katika kufanya tathmini inayozingatia thamani halisi ya fedha (value for money) ya Miradi Mikubwa.

3. Kamati inaishauri Wiazara ya Fedha itowe taaluma kwa wananchi juu ya dhana ya ukuaji wa uchumi sambamba na kuwapatia mafunzo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kwa kuwa wananchi walio wengi hawaielewi dhana hiyo kwa kuilinganisha na hali ya kipato wanachokipata.

4. Ili kuhakikisha misamaha ya Kodi wanayopatiwa wafanyabiashara kwa lengo la kuwapa unafuu wananchi inatumika ipasavyo, Kamati inashauri Serikali ifuatilie bei za bidhaa na kuwachukulia hatua wafanyabiashara wanaoitumia vibaya misamaha hiyo.

5. Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango ifanye utafiti katika sekta mbali mbali hususan sekta ya kilimo na utalii, ili kuweza kutambua uhusiano uliopo katika sekta hizi na kuwawezesha wananchi kunufaika nazo, ikiwemo suala la wakulima kuyatumia masoko ya utalii pamoja na ajira.

6. Kamati inaishauri Serikali kuwa makini juu ya fedha inayopelekwa kutekeleza Miradi ya Mabadiliko ya Tabia nchi, kwani hali ilivyo sasa, inaonekana kuna mabadiliko makubwa ya hali ya hewa, hivyo ni muhimu fedha zinazolengwa kutumika katika miradi hiyo zikafuatiliwa kwa kina iwapo zinaleta tija inayokusudiwa.

7. Kamati inaishauri Serikali kufanya utafiti wa kina juu ya sekta ya utalii, ili kuona ni kwa kiasi gani wananchi hususan walio katika maeneo ya uekezaji wa mahoteli wananufaika na sekta hii, ili dhana ya utalii kwa wote iwe na uhalisia. Pia Serikali kupitia Wizara husika ihakikishe waekezaji wa Hoteli wanatimiza masharti ya uajiri kwa kuweka kipaumbele kwa wazawa hususani kwa kazi ambazo hazihitaji utalaamu maalum.

## BENKI KUU YA TANZANIA (BOT) TAWI LA ZANZIBAR

Benki Kuu ya Tanzania ilianzishwa mwaka 1966 kwa Sheria iliyopitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (The Bank of Tanzania Act 1966). Jukumu kuu la Benki Kuu ni kuandaa na kutekeleza sera ya fedha inayolenga kutunza thamani ya fedha na kudhibiti mfumuko wa bei ili kuchochea ukuaji wa uchumi . Katika Kuishauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Benki kuu hufanya tafiti katika sekta mbali mbali za kiuchumi na miongoni mwa maeneo ambayo Benki Kuu imefanya utafiti na kutoa Mapendekezo yake ni pamoja na Utafiti wa thamani ya uzalishaji na uuzaji wa mwani mwaka 2014 na Utafiti wa Maendeleo ya Matarajio ya Sekta ya Utalii mwaka 2015.

Jukumu la Benki Kuu ya Tanzania kupitia Tawi lake la Zanzibar ni Kutekeleza kazi za msingi za Benki Kuu ikiwa ni pamoja na kuhifadhi akiba za Benki za Biashara na kuishauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhusiana na mambo ya fedha na uchumi. Kamati ilifanya ziara Katika Benki Kuu Tawi la Zanzibar kwa lengo la kupatiwa taarifa juu ya Utekelezaji wa Majukumu yake.

## CHANGAMOTO ZA BENKI KUU TAWI LA ZANZIBAR

1. Baadhi ya wananchi kukosa uelewa mzuri kuhusu kazi na majukumu ya Benki Kuu ya Tanzania.

2. Baadhi ya wananchi kukosa uelewa mzuri kuhusu fursa za uwekezaji katika masoko ya fedha, hii ni kutokana na ushiriki mdogo wa wananchi wa Zanzibar katika uwekezaji kwenye dhamana za Serikali na hati fungani (Tressury Bill na Tressury Bonds).

3. Baadhi ya wananchi kukosa uelewa wa kutosha juu ya kuzitambua noti halali ili kuepukana na upokeaji noti bandia.

4. Wananchi na wafanyabiashara kupendelea kufanya mauziano ya bidhaa na huduma kwa fedha taslimu.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Ili kukabiliana na Changamoto ya uelewa mdogo wa wananchi kuhusu Majukumu ya Benki Kuu, Kamati inashauri Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipangokuwaelimisha wananchi juu ya majukumu ya benki hiyo. Aidha, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wapatiwe mafunzo maalum yatakayowawezesha kufahamu majukumu ya Benki hiyo, mafanikio pamoja na changamoto zake.

2. Kutokana na kuwepo kwa tatizo la kuchelewa kupata baadhi ya taarifa muhimu za fedha kwa Benki kuu - Tawi la Zanzibar zinazohusu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Kamati imeona kuna haja ya Wizara ya Fedha na Mipango Zanzibar kufanya mazungumzo na Benki kuu juu ya utaratibu mzima utakaowezesha Benki kuu tawi la Zanzibar kupata taarifa kwa haraka.

## MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR – ZSSF

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar umeanzishwa chini ya Sheria namba 2 ya mwaka 1998, kwa lengo la kuwahifadhi wanachama wake wanapopatwa na majanga ambayo husitisha au hupunguza kipato chao kwa sababu mbali mbali kama vile uzee, ulemavu maradhi au kifo pamoja na majanga mengine yaliyoainishwa katika Sheria hiyo.

Jumla ya wanachama 81,477 wameasajiliwa pamoja na uekezaji wa miradi 8 mikubwa umefanyika, miradi mitano kati ya hiyo imekamilika. Miradi iliyokamilika ni pamoja na Hoteli na Afisi ya ZSSF Tibirinzi Pemba, kituo cha biashara Mwanakwerekwe, kiwanja cha kufurahishia watoto Kariakoo, kiwanja cha watoto Umoja, na Mnara wa kumbukumbu ya miaka 50 ya Mapinduzi na bustani ya Michenzani. Aidha miradi inayoendelea ni mradi wa ujenzi wa nyumba za makaazi Mbweni, ukarabati wa jumba la Treni na ujenzi wa maduka (Shopping mall) Michenzani Zanzibar ambao upo katika hatua za awali. (*Angalia kiambatanisho namba 1 kinachoonesha uchanganuzi wa mapato na matumizi ya miradi iliyokamilika)*

Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji iliyojumuisha mafanikio, changamoto na muelekeo wa Mfuko na kufanya ziara ya kukagua baadhi ya miradi hiyo.

### CHANGAMOTO ZA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII

1. Kwa kipindi kirefu mfuko umekosa wabia wa kushirikiana nao katika uwekezaji wa miradi mikubwa kwa lengo la kugawana tija na athari za miradi inayowekezwa.

   Hali hii imepelekea Mfuko kutumia mtaji wake pekee katika miradi hiyo ambapo ni hatari kwa uekezaji mkubwa.

2. Kukosekana soko la majengo ya uekezaji yanayojengwa na Mfuko kwa upande wa Zanzibar, ambapo mara nyingi majengo hukodishwa kwa kodi ndogo, au kukosa wakodishwaji kabisa hali inayoathiri tija za miradi na kuendeshwa kwa hasara.

3. Kuongezeka kwa gharama za miradi kunakotokana na ugumu wa upatikanaji wa mchanga na vifaa vyengine vya ujenzi kunaathiri utekelezaji wa miradi hiyo.

4. kukosekana kwa utaalamu wa usimamizi na uwendeshaji miradi iliyowekezwa na mfuko hali inayopelekea mradi kama wa kiwanja cha watoto - Uhuru kuendeshwa na wafanyakazi wa kawaida wa Mfuko ambao kimsingi si weledi katika kuendesha miradi ya namna hiyo.

5. Kutokuwepo kwa mfumo wa kisasa katika makusanyo ya fedha kutoka katika miradi ya viwanja vya kufurahishia watoto Kariakoo na Tibirinzi Pemba, ambapo kwa mfumo uliopo sasa wa kukusanya fedha mikononi kunapelekea mianya ya kuvuja kwa mapato.

6. Mabadiliko ya Sheria ya Utumishi wa Umma namba 2 ya mwaka 2011 yanayotokana na Sheria ya Mabadiliko ya Sheria Mbali Mbali namba 1 ya 2018, yanaathiriri uendeshaji wa Mfuko wa ZSSF katika kutoa huduma kwa wanachama wake. Sheria hiyo inapokonya baadhi ya madaraka ya Mfuko, na hivyo kuondosha mantiki ya kuwa na Bodi ya Mfuko huo. Aidha, baadhi ya maelekezo yanayotolewa na vyombo vyengine vya Serikali yanaweza kuathiri utendaji wa Mfuko huo.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inashauri Mfuko wa ZSSF kubadilisha mbinu za kutafuta wabia wa kibiashara pamoja na kutangaza mafanikio waliyoyapata katika miradi iliyokamilika kwa lengo la kuwavutia wabia hao, sambamba na kuhakikisha wanafanya uekezaji katika miradi yenye ina soko kwa upande wa Zanzibar.

2. Kwa lengo la kupata wateja na kutanua wigo katika soko, Kamati inashauri Mfuko wa ZSSF kutangaza zaidi fursa zilizopo katika miradi yake iliyokwisha kamilika, ili kupata wafanyabiashara ambao wataweza kuunga mkono jitihada za Mfuko huo na hatimae kuongeza tija katika baadhi ya miradi ambayo kwa sasa inaonekana kuendeshwa kwa hasara. Aidha, Kamati inaishauri ZSSF kutafuta soko la majengo yake ya miradi ya nyumba za makaazi kupitia “Diaspora” ambao wanauhitaji mkubwa wa nyumba hizo.

3. Kwa lengo la kupunguza gharama za miradi inayoendelea kujengwa na Mfuko, Kamati inashauri Mamlaka inayohusina na upatikanaji wa mchanga, kuipa kipaumbele miradi mikubwa inayoendelea nchini kwa kuiwezesha kupata mali

ghafi ya mchanga haraka kadri itakavyokuwa inahitajika kwa lengo la kuiwezesha miradi hiyo kumaliza kwa wakati.

4. Ili kudhibiti mapato yanayotokana na uekezaji katika viwanja vya kufurahishia watoto, Kamati inashauri Mfuko uharakishe mchakato wa kuanza kutumia mfumo wa kisasa wa kukusanya mapato utakaowezesha fedha hizo kuingia moja kwa moja kwenye akaunti ya Mfuko.

## MAMLAKA YA UEKEZAJI NA UKUZAJI VITEGA UCHUMI ZANZIBAR-ZIPA

Katika kuzingatia umuhimu na mchango wa uekezaji katika suala zima la ukuaji wa uchumi, Kamati ya Bajeti imelitazama kwa ukaribu mkubwa suala hilo kupitia Mamlaka ya Uekezaji na Vitega Uchumi **ZIPA** ambayo kwa Zanzibar ndiyo yenye jukumu la moja kwa moja la kusimamia vitega uchumi kwa mujibu wa sheria namba 11 ya mwaka 2004 ambayo imeanzisha Mamlaka hiyo.

Kamati ya Bajeti pamoja na ziara mbali mbali kupitia **ZIPA** katika miradi ambayo inaisimamia, pia ilipata fursa ya kufanya majadiliano juu ya utendaji kazi wa Mamlaka hiyo ikiwa ni pamoja na mafanikio na changamoto.

## CHANGAMOTO ZA MAMLAKA YA UWEKEZAJI NA UKUZAJI VITEGA UCHUMI

1. Kutokukamilika huduma za ***“One Stop Center”*** ambazo zitamuwezesha muekezaji kumaliza mahitaji yake yote yanayohusiana na uwekezaji katika eneo moja, kwa lengo la kurahisisha mchakato mzima wa uekezaji. Kukosekana kwa huduma hizi kunapelekea utaratibu mzima wa hatua zinazopaswa kufuatwa na waekezaji kuwa si rafiki na kusababisha usumbufu usio wa lazima na mara nyengine kutoa mwanya kwa vitendo vya rushwa.

2. Mamlaka kukosa usafiri wa gari kwa muda mrefu ambao unahitajika kwa shughuli za ufuatiliaji wa maendeleo ya miradi mbali mbali kwenye maeneo tofauti ambayo Mamlaka imeyatolea vibali vya uekezaji.

3. Kukosekana kwa ‘Master Plan’ kwa ajili ya ujenzi wa miji au sehemu za kibiashara kunapelekea kuchelewa kutolewa kwa vibali vya ujenzi wa miradi mbali mbali kunakolalamikiwa na waekezaji mara baada ya kupata vibali vya uekezaji kutoka **ZIPA**.

4. Kuwepo kwa watu wa kati (madalali) ambao mara nyingi huwa wanatumiwa na waekezaji wa kigeni, ambapo mara nyengine hutoa taarifa zisizo na usahihi kwa wawekezaji hao katika hatua za awali na kupelekea waingie gharama kubwa katika hatua hizo , na hata

kukwama katika hatua za awali kutokana na kutumia njia za mkato katika mchakato wa uekezaji.

5. Kamati imebaini kukwama kwa miradi mingi ya waekezaji katika sekta ya uvuvi, hali inayowarejesha nyuma wawekezaji wa ndani na wa nje katika sekta hii. Kamati imepatiwa taarifa hiyo na Mamlaka ya **ZIPA** kuwa jumla ya miradi 8 inayohusiana na shughuli za uvuvi iliripotiwa kukwama.

6. Kamati imeweza kufahamu mitazamo tofauti ya wananchi katika maeneo ambayo miradi mikubwa inakusudiwa kuekezwa, kunakotokana na hofu ya wananchi katika maeneo hayo, kuhusiana na maendeleo na athari zake kwa mustakbali na utamaduni wao pamoja na kuhamishwa katika maeneo ambayo wameshajenga makaazi yao ya kudumu.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaishauri Serikali katika Bajeti ya mwaka wa fedha **2018/2019** kulipa kipaumbele suala la kuipatia fedha Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi-**ZIPA** kwa lengo la kufanya manunuzi ya gari itakayoiwezesha Mamlaka hiyo kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ikiwa ni pamoja na kufuatilia miradi iliyoidhinishwa kwa ustawi wa maendeleo ya Zanzibar.

2. Kamati inashauri Serikali kupitia **ZIPA** kulipa uzito suala la "***one stop center***" kwa kuimarisha huduma hiyo, ili kurahisisha mazingira ya mchakato wa uekezaji nchini, ukizingatia ukweli kuwa, suala hilo limeshakua likizungumzwa kwa muda mrefu bila ya kufanyiwa kazi. Aidha, kuimarisha huduma za "***one stop center"*** kutaepusha kuwepo kwa madalali wa wawekezaji ambao wanaipa taswira mbaya Mamlaka ya uwekezaji **ZIPA.**

3. Kutokana na umuhimu wa sekta ya uvivu kwa Zanzibar na mchango wake katika kuinua hali za uchumi wa wananchi walio wengi, Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo Maliasili Mifugo na Uvuvi kwa kushirikaiana na **ZIPA** kuitafutia Ufumbuzi changamoto ya Miradi ya Uvuvi ambayo imekwama utekelezaji wake.

## MAENEO HURU YA UWEKEZAJI AMANI

Kamati ilipata fursa ya kutembelea maeneo ya Viwanda vidogo vidogo-Amaani ikiwa ni moja ya maeneo ya uwekezaji yaliyotengwa na Serikali na kuimarishwa kwa lengo la kuendeleza wawekezji wa ndani na wa nje wa viwanda vidogo vidogo. Kamati ilipata fursa ya kuzunguka eneo hilo na kuhoji baadhi ya mambo pamoja na kuomba kupatiwa baadhi ya nyaraka muhimu zinazohusiana na wawekezaji wenye kuhodhi maeneo hayo.

## CHANGAMOTO ZA MAENEO HURU YA UEKEZAJI - AMANI

1. Kuwepo kwa majengo yaliyotengwa kwa ajili ya wawekezaji ambayo hayajatumika kwa muda mrefu na hivyo kuikosesha mapato Mamlaka na Serikali kwa ujumla.

2. Kuchakaa na kuvuja kwa majengo yaliyopo maeneo ya uwekezaji hali iliyochangiwa na kutofanyiwa ukarabati kwa muda mrefu.

3. Kubomoko kwa uzio wa eneo la Amani kunakohatarisha usalama wa eneo la viwanda vidogo vidogo pamoja na mali za wawekezaji wengine wanaofanya shughuli zao katika eneo hilo kwani wananchi huingia katika eneo hilo bila ya kuzingatia taratibu na kukaribisha uvamizi wa maeneo ya uwekezaji kwa kujenga makaazi yaliyo jirani sana na eneo hilo.

4. Kuwepo kwa makontena yaliyokaa kwa muda mrefu na kuchakaa bila ya kutumika na kutofahamika mmiliki wake.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

**1.** Kwa kuwa suala la ulinzi wa maeneo ya uwekezaji ni la muhimu sana, na kwa vile ZIPA haiwezi kuufanyia marekebisho uzio wa eneo la Viwanda vidogo vidogo liliopo Amani kwa gharama zao kutokana na ukubwa wake (milioni 80 kwa km 20), Kamati inaishauri Serikali kuipatia fedha ZIPA katika Bajeti ya 2018/19 kwa lengo la kuujenga uzio huo na kuweza kuzihifadhi vyema mali zilizomo katika eneo hilo.

2. Kamati inaishauri ZIPA ifikirie namna ya kuyaendeleza majengo ambayo hayajatumika kwa muda mrefu na kuwapatia wawekezaji wengine waliotayari kufanya uwekezaji katika majengo hayo kwa lengo la kuipatia Serikali mapato.

3. Kamati inaishauri ZIPA kuandaa mpango endelevu wa kuyakarabati majengo yaliyo ndani ya eneo la uwekezaji Amani kwa kuyafanyia matengenezo madogo madogo kila baada ya muda kwa lengo la kuyatunza na kuiepushia Serikali gharama kubwa iwapo majengo hayo yataenedelea kukaa kwa muda mrefu bila ya kufanyiwa ukarabati.

**4.** Kwa lengo la kuisogeza ZIPA karibu na wawekezaji katika eneo la uwekezaji Amani, Kamati inaishauri ZIPA, kufikiria uwezekano wa kufungua ofisi ndogo katika eneo hilo, ambayo itaweza kusaidia kufahamu mambo mbali mbali yanayoendelea katika eneo hilo.

**PENNY ROYAL (GIBBRALTAR) ZANZIBAR LTD**

Mradi wa Penny Royal ni mradi mkubwa unaotarajiwa kuleta fursa kubwa ya ajira tokea kuanzishwa kwake hadi wakati wa utoaji wa huduma. Kamati imepata fursa ya kutembelea eneo la mradi na kukutana na wahusika wa mradi huo. Kamati imearifiwa kuwa Mradi wa Penny Royal unatarajiwa kugharimu jumla ya dola za kimarekani bilioni mbili. Mbali na ajira ambazo wananchi watafaidika nazo, jamii pia kupitia programu mbali mbali ambazo zitakuwa

zikisimamiwa na mradi huu kama ***"Best of Zanzibar"*** ambayo itakusanya nyanja mbali mbali za jamii ikiwa ni pamoja na wajasiriamali, elimu na usalama wa wananchi wenyewe.

## CHANGAMOTO ZINAZOUKABILI MRADI WA PENNY ROYAL

1. Kuwepo kwa mvutano na mkwamo wa mradi huo unaosababishwa na mgogoro wa ardhi uliopo baina ya muekezaji na Serikali kupitia Wizara ya Ardhi Maji Nishati na Mazingira, ambapo muekezaji amekuwa akihitaji eneo zaidi kwa ajili ya utanuzi wa mradi huo linalokisiwa kuwa na ukubwa wa hekta **220,** suala ambalo halikukubaliwa moja kwa moja na Serikali licha ya muekezaji kuhakikishiwa upatikanaji wa eneo hilo baada ya kuliendeleza eneo la ardhi ambalo ameshakabidhiwa, hatua ambayo kimsingi haikumridhisha muekezaji. Changamoto hii inapelekea kusuasua kwa mradi huo na kuongezeka kwa gharama za uendelezaji wa eneo husika.

2. Kukosekana kwa Mpango Mji wa nchi na wa Mkoa wa Kaskazini kunapelekea Serikali kuchelewa ama kusita kufanya baadhi ya maamuzi juu ya aina ya uwekezaji na maboresho ya miundo mbinu inayokusudiwa kufanyika.

3. Fidia kubwa inayodaiwa na wananchi katika eneo la uwekezaji ambalo lina vipando au mazao, ikiwa ni pamoja na minazi ambapo wananchi wamekua wakidai fidia ya jumla ya Shilingi milioni nne kwa mnazi mmoja gharama ambazo si halisia.

4. Wananchi kudai fidia katika eneo ambalo wawekezaji wamepatiwa na Serikali bila ya kuwa na stakabadhi yoyote ya eneo hilo, licha ya wawekezaji kueleza kuwa tayari wameshawahi kutoa fidia katika eneo hilo katika kipindi cha nyuma.

5. Tabia ya uvamizi wa eneo la mradi kunakofanywa na wakaazi wa karibu na eneo hilo, ambao huingia kwa shuguli zao za kujitafutia mahitaji yao ya kila siku kama kukata kuni, suala ambalo linawakwaza wawekezaji kwa kua kuna shughuli za ujenzi zinazoendelea ambazo zinaweza kuhatarisha maisha ya wananchi hao pindi watakapokuwa katika eneo la kazi bila ya taarifa.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Kwa mujibu wa taarifa za muekezaji na Serikali, Kamati inashauri mamlaka husika kuliangalia upya suala la kumuongezea ardhi ya hekta 220 muekezaji, kwa kuzingatia umuhimu wa mradi husika na faida inayoweza kupatikana kwa wananchi kupitia mradi huo. Kutokuongezwa eneo hilo kutapelekea kuongezeka kwa gharama za mradi huo.

2. Kamati inaishauri Wizara husika kupitia Serikali ya Mkoa huo, kutoa tamko rasmini juu ya umiliki wa eneo hilo la uwekezaji ili kuepusha wimbi la wananchi wanaokwenda kudai fidia katika eneo hilo la uekezaji.

3. Kamati inaishauri Serikali kuu kuharakisha mchakato wa kuandaa Mpango Mji Mkuu, kutokuwepo kwa mpango huo kunapeleeka kuibuka kwa changamoto mbali mbali hususan kwa wawekezaji wakubwa kwa kile kinachoelezwa kuwa, kutofahamika kwa mipango ya baadae ya Serikali katika maeneo mbali mbali, hali ambayo pia hupelekea urasimu juu ya maamuzi ya ardhi na hatimae kuzorotesha shughuli za uekezaji.

## MAENEO HURU YA UEKEZAJI FUMBA

Kamati ya Bajeti pia katika kutekeleza majukumu yake ilipata fursa ya kufanya ziara ya kuona maendeleo ya mradi wa nyumba za Fumba ambao upo chini ya kampuni ya Bakhresa (Bakhresa Group of Company). Mradi huo utahusisha nyumba za kuishi pamoja na ujenzi wa miundombinu, ikiwemo barabara, viwanja vya michezo, maduka makubwa (Shoping Mall). Aidha, Kamati iliarifiwa kwamba kwa awamu ya kwanza jumla ya nyumba 152 zitajengwa kwa ajili ya wananchi wa kipato cha kati na juu.

## CHANGAMOTO ZA MRADI

1. Kukosekana kwa barabara ya moja kwa moja na yenye masafa mafupi inayouunganisha mji mpya wa Fumba na Uwanja wa ndege, ambapo Kamati imeelezwa kuwa Serikali imeahidi kujenga kilomita 2 za barabara hiyo inayokisiwa kuwa wa urefu wa kilomita 8 na muekezaji atajenge kilomita 6 zitakazobakia kukamilisha kilomita 8

2. Gharama kubwa ya mradi huo wa mji wa Fumba itatumika katika kuimarisha miundo mbinu ya msingi kwa kuwa eneo hilo halikua na miundo mbinu ya msingi wakati wa kuanzishwa kwake. Hali itakayosababisha nyumba za mradi katika mji huo kuwa ghali sana kiasi cha mwananchi wa kawaida kushindwa kumiliki.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inashauri kutokana na kasi ya ujenzi wa mradi wa Fumba, Serikali ichukue hatua za haraka kuanza ujenzi wa barabara itakayouunganisha mji huo na Uwanja wa ndege ili kwenda sambamba na kasi ya mradi.

2. Kamati inaishauri Serikali kupitia Mamlaka ya **ZIPA** ambayo ndio inayosimamia masuala ya uekezaji Zanzibar, kuimarisha miundo mbinu ya msingi katika maeneo ya uekezaji kwa lengo la kuwavutia waekezaji wenye nia ya kuekeza Zanzibar lakini wanarudhishwa nyuma kutokana na kukosekana kwa miundo mbinu ya msingi ambayo huongeza gharama za uekezaji.

3. Kutokana na ukuaji wa mji wa Zanzibar unaokwenda sambamba na ongezeko la watu, Kamati inaishauri Mamlaka ya **ZIPA** kwa kushirikian na Shirika la Nyumba la Zanzibar kufikiria mradi wa nyumba za maendeleo ambazo zitakua zimejengwa kisasa na kwa gharama nafuu kwa lengo la kuwawezesha wananchi wenye kipato cha kawaida kumudu gharama za nyumba hizo.

## ZIARA YA KAMATI KATIKA MAMLAKA YA KUENDELEZA MAENEO YA UZALISHAJI KWA MAUZO YA NJE (EXPORT PROCESSING ZONE AUTHORITY-EPZA) UBUNGO- DAR ES SALAAM

Kamati ya Bajeti ilifanya ziara ya kujifunza katika **Mamlaka ya Kuendeleza Maeneo ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (Export Processing Zone Authority-EPZA)** tarehe 20/09/2017 hadi tarehe 21/09/2017. Katika ziara hiyo, Kamati ilipata fursa ya kutembelea maeneo ya uwekezaji ya Tooku Garments Production Centres, Tooku skills Training Centres na Quality Pulse Factory.

Kamati imejifunza namna Wawekezaji (Tooku Garments Production Centres na Tooku Skills Training Centre) wanavyowapatia fursa za mafunzo na ajira kwa vijana, hali inayosaidia kuinua kipato cha wananchi na kujifunza maarifa mapya. Kwa msingi huo Kamati imeshauri wawekezaji wa viwanda vilivyopo katika maeneo ya EPZA kuja kutembelea na kufanya utafiti Zanzibar ili kuangalia uwezekano wa kuekeza viwanda-Zanzibar, na kusaidia kuinua soko la ajira pamoja na mapato ya Serikali.

Kamati pia imejifunza namna kituo cha "***one stop center***" kinavyofanya kazi, ambapo pamoja na changamoto ndogo ndogo za mifumo ya kiutawala inayoathiri masuala ya maamuzi, Kamati iliarifiwa kwamba, takribani huduma zote za uekezaji zinapatikana kupitia maafisa waliopo kituoni hapo.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Mamlaka ya ZIPA izidishe mashirikiano na Mamlaka ya EPZ ili kupata fursa ya kubadilishana uzoefu baina ya pande mbili katika kuibua mbinu bora za kukuza uwekezaji Zanzibar.

2. Ili kukabiliana na changamoto ya miradi ambayo haijaendelezwa kwa muda mrefu, ZIPA iangalie uwezekano wa kutumia masharti ya uekezaji yanayomshurutisha muekezaji kuwa na mtaji wa kutosha kabla ya kuanza uwekezaji.

3. Ili kukuza ufanisi wa huduma za "***one stop centre***" katika Mamlaka ya ZIPA, ni vyema ZIPA wakaweka mfumo wa ***kielektroniki*** wa kujaza taarifa za waekezaji ambao utaruhusu taasisi zote zilizopo ZIPA katika kitengo cha "***One Stop Centre"*** kuona taarifa muhimu za muekezaji moja kwa moja kwa njia ya mtandao,ili kupunguza usumbufu wa kuwahoji wawekezaji masuala ambayo yanajirejea.

4. Katika kuanzisha maeneo huru ya uwekezaji ni vyema ikazingatiwa kuweka eneo la huduma za kifedha katika ***"Master Plan"*** ya maeneo hayo, hii ni kutokana na umuhimu wa huduma hizo hususan katika maeneo ya viwanda.

## ZIARA ZA MAFUNZO KWA KAMATI YA BAJETI DAR ES SALAAM

Katika kutekeleza majukumu yake Kamati ilipata fursa ya kufanya ziara jijini Dar es Salaam kwa lengo la kujifunza na kupata taarifa muhimu za Kiuchumi na Mapato kutoka Wizara ya Fedha na Mipango ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Tume ya Pamoja ya Fedha (Joint Finance Commission).

## WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Kamati ilifanya ziara katika Wizara hii kwa lengo la ziara kujifunza na kupata taarifa kuhusiana na mgawanyo wa Fedha za Muungano na Misaada ya Kibajeti (GBS) baina ya pande mbili za Muungano (Tanzania Bara na Zanzibar). Aidha, katika Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Kamati ilipata taarifa na kujifunza juu ya matumizi ya mashine za kutolea risiti (EFD) ambapo kwa upande wa Zanzibar katika mkakati wake wa kuimarisha mapato ni pamoja na kuanza kutumia mashine hizo katika kukusanya mapato yake. Kamati pia ilipata fursa ya kutembelea Tume ya Pamoja ya Fedha (Joint Finance Committee - JFC) ambayo imeundwa kwa mujibu wa kifungu cha 134 cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na kwa kupitia Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha ya mwaka 1996, Sura 140. Kamati iliweza kujifunza majukumu ya Tume, changamoto na mafanikio yaliyopatikana tokea kuanzishwa kwake.

## MGAWANYO WA FEDHA ZA MUUNGANO NA MISAADA YA KIBAJETI

Kuhusiana na mgawanyo wa Fedha za Muungano na Misaada ya Kibajeti Kamati iliweza kufahamu yafuatayo:

1. Fedha za Misaada ya Kibajeti (GBS) zimekuwa zikipungua kwa kiasi kikubwa kutokana na masharti yanayotolewa na wahisani, na mara nyengine kutopatikana kabisa kwa fedha hizo hali inayopelekea kuzorota kwa utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa ujumla. Aidha, katika mwaka wa Fedha 2017/2018 hakuna fedha yoyote ya GBS iliyopatikana.

2. Kamati imeweza kufahamu kuwa utaratibu unaotumika katika kugawana fedha za Muungano na misaada ya kibajeti hadi sasa ni ule wa 4.5% kwa Zanzibar, utaratibu ambao umerithiwa kutoka katika utaratibu uliowekwa kwa muda " interim agreement" wa kugawana faida ya gawio la Benki Kuu ya Tanzania (BOT) baina ya Tanzania Bara na Zanzibar,baada ya kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

3. Kuhusiana na changamoto zilizopo katika kodi baina ya Tanzania Bara na Zanzibar hususan katika kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ambayo kwa wafanyabiashara wa Zanzibar wamekuwa wakilipa kodi hiyo mara mbili kwa upande wa Tanzania Bara na Zanzibar iwapo bidhaa zitakuwa zinatoka Tanzania bara, Kamati imepata kufahamu kuwa changamoto hii inasababishwa na sera za kodi zilizopo baina ya pande mbili, hivyo tatizo hili linaweza kuzungumzwa na kutafutiwa ufumbuzi.

**MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA - TRA DAR ES SALAAM**

Itakubukwa kwamba Serikali ya SMZ ilipanga kuanza kutumia Mashine za EFD kwa lengo la kuimarisha ukusanyaji wa mapato. Hivyo, Kamati ya Bajeti iliona ni busara kwenda kujifunza kuhusu matumizi ya mashine hizo kwa lengo la kuishauri vyema Serikali ya SMZ kuhusu utekelazaji wake. Kamati ilipokea maelezo ya kina kuhusiana na mashine za EFD kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), ambapo Kamati iliarifiwa awali kabla mashine hizo kuanza kutumika kodi iliyokusanywa ilitokana na mauzo ya jumla yanayopatikana kwa biashara husika, hata hivyo, kulikuwa na changamoto kwa wafanyabiashara kutotowa takwimu sahihi ya mauzo yao. Kutokupatikana kwa takwimu sahihi, kulipeleka mashine ya EFD kuanza kutumika. Kutumika kwa mashine hizo kulihakikisha kuwa mfanyabiasha anafanya usajili na kupata namba yake maalum ya kufanya malipo (Pay Identification Number), kuwasilisha taarifa zake za kodi, kulipa kodi kwa wakati na taarifa zinazowasilishwa zinazohusiana na kodi zipo kwa usahihi.

Kuhusiana na matumizi ya mashine za kutolea risiti (EFD), Kamati iliweza kujifunza mambo mbali mbali na inashauri Serikali juu ya mambo yafuatayo:-

1. Katika hatua za awali za kupata mashine za EFD kutoka kwa watengenezaji, ni vyema Serikali kupitia Wizara husika, ikaweka umakini wa hali ya juu katika kupendekeza sifa za mashine hizo " specification", kwani, uteuzi wa sifa hizo ni suala la msingi sana katika kuhakikisha kunapatikana mashine ambazo zitakuwa na sifa zinazolingana na mahitaji na mazingira halisi ya ukusanyaji kodi

2. Kamati inashauri kuwa taasisi inayosimamia mapato iwe na jukumu la kununuwa mashine za EFD pamoja na kuzisimamia. Aidha, katika kulifanikisha jambo hili, kunahitajika uwekezaji mkubwa ikiwemo kuweza kumudu kununuwa mashine hizo pamoja na kuwapa mafunzo wataalamu ya kuweza kuzisimamia ipasavyo matumizi yake.

3. Kamati inaishauri Seriklai kuwa wakati wa kuanza kutumia mashine za EFD suala la kuwadhibiti wataalamu " technicians" lipewe kipaumbele, kwa vile wataalamu

wasiokuwa waaminifu wanaweza kushirikiana na wafanyabiashara na hatimae kufanya udanganyifu utakaopelekea kupoteza mapato ya Serikali.

4. Kamati inaishauri Serikali juu ya kuzingatia ubora wa risiti zinazotarajiwa kutumika katika mashine za EFD. Kwa mujibu wa taratibu za kodi, risiti ya mauzo inapotelewa inatakiwa kudumu kwa muda wa miaka mitano kabla ya kuharibika. Kamati iliarifiwa kuwa, kwa upande wa mashine za EFD zilizoanza kutumika Tanzania Bara, risiti zinazotolewa katika mashine hizo zinafutika kwa haraka. Katika kukabiliana na tatizo hilo Kamati inashauri wakati wa kutafuta msambazaji kwa upande wa Zanzibar ni muhimu kukubaliana na msambazaji ambaye ataweza kuhakikisha ubora wa risiti zake zitakazoweza kudumu kwa kipindi kirefu.

5. Kamati iliarifiwa kuwa mashine za EFD zilipoanza kutumika, hazikukubaliwa moja kwa moja na wafanyabiashara kwa upande wa Tanzania Bara. Kwa kulizingatia hili, Kamati inaishauri Serikali ili kuweza kukabiliana na tatizo hili ni vyema elimu ikatolewa mapema juu ya umuhimu wa matumizi ya mashine hizo kupitia jumuiya za kibiashara ambazo zinakuwa na ushawishi mkubwa kwa wafanyabiashara wengine.

6. Kamati ilipata uelewa kuwa matumizi ya mashine za EFD yataisaidia Serikali katika kupata taarifa sahihi za mauzo ya wafanyabiashara mbali mbali, kwa vile kumbukumbu za mauzo hayo zikishaingizwa zinakuwa za kudumu na haziwezi kufutwa na zinakwenda moja kwa moja katika mfumo wa rikodi ya mauzo ulioandaliwa. Kwa kuwa mchakato wa kuanza kutumia mshine za EFD umeshakuwa wa muda mrefu, Kamati inashauri Serikali kuharakisha mchakato huo.

## TUME YA PAMOJA YA FEDHA (JOINT FINANCE COMMISSION- JFC)

Kamati ilipokea taarifa juu ya majukumu ya Tume ya Pamoja ya Fedha ambayo yameanishwa katika Ibara ya 134(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ambayo ni pamoja na;

Kuchambua mapato na matumizi yanayotokana na, au yanayohusu utekelezaji wa mambo ya Muungano na kutoa mapendekezo kwa Serikali mbili kuhusu mchango na mgao wa kila moja wapo wa Serikali hizo. Uchambuzi wa mapato na matumizi umeekewa msingi chini ya Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha, Sura 140, kifungu cha 11(1) ambapo kumetaja Sekretarieti ya Tume ambayo ndio chombo kinachochambua na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Tume kuhusiana na masuala mbali mbali ya Uhusiano wa kifedha baina ya Serikali mbili.

Kamati imepata kufahamu kuwa Tume ya pamoja ya Fedha kwa kipindi cha kuanzia Machi 2003 hadi Juni, 2017 imefanya stadi ya uchambuzi wa kubainisha Wizara na Asasi za Muungano na Gharama za kuendesha mambo hayo, Stadi ya Usimamizi wa Deni la Taifa baina ya SMT na SMZ, Stadi ya kubainisha mfumo bora wa kodi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Stadi kuhusu mwenendo wa uchumi na mapato ya muungano na kuweza kutolewa mapendekezo mbali

mbali kuhusiana na stadi hizo ambapo licha ya Tume kutowa mapendekezo hayo, utekelezaji wa mapendekezo hayo kwa SMT na SMZ umekuwa unachelewa kutolewa uamuzi.

Kamati imeweza kubaini kuwa Tume ya Pamoja ya Fedha inakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa fedha hali inayoathiri utekelezaji wa majukumu ya Tume hiyo ingawaje Tume katika kukabiliana na changamoto hiyo, imewasilisha maombi kwa Wizara ya Fedha ya SMT ili kuongezewa Bajeti pamoja na kupatiwa fedha hizo kwa mujibu wa kiwango kilichoidhinishwa.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Kiujumla Kamati ya Bajeti imejifunza na kufahamu changamoto na mafanikio ya Tume hiyo. Hivyo, Kamati inashauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia vikao vyao mbali mbali kuona namna ya mapendekezo yanayotolewa na Tume ikiwemo vigezo vya kugawana mapato na kuchangia gharama za Muungano na Muongozo wa Uendeshaji wa Akaunti ya Fedha ya pamoja yanavyoweza kutekelezwa.

## SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA ZANZIBAR - ZSTC

Shirika la Bishara la Taifa ZSTC linatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Namba 11 ya mwaka 2011 ya shirika hilo. Kamati ilipokea taarifa ya Shirika la ZSTC kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Shirika hilo ikiwa ni pamoja na kununua, kuuza karafuu pamoja na mazao mengine ya kilimo kwa bei ya ushindani, kulinda ubora wa mazao ya karafuu na mazao ya kilimo, kufanya usarifu, kuongeza thamani pamoja na kutafuta masoko ya mazao. Aidha Kamati ilitembelea ghala la kuhifadhia karafuu liliopo Bandarini - Malindi kwa lengo la kuona mazingira ya ghala hilo na ubora wake

## CHANGAMOTO ZA SHIRIKA

**1.** Uchakavu wa maghala ya shirika. Shirika linamiliki maghala ambayo yanahitaji kufanyiwa ukarabati ili yaweze kutumika kama vianzio vya mapato ambapo muenekano wa sasa wa baadhi ya maghala hayo hauridhishi, hali hii hupelekea shirika kukosa fedha za kukodisha maghala hayo kwa bei nzuri.

**2.** Mashine zinazotumika katika kusafisha karafuu katika maghala ni za kizamani sana, kutokuwa na mashine za kisasa kunaweza kupunguza ubora wa Karafuu.

**3.** Kuwepo kwa taarifa zisizo na usahihi zinazotolewa na wakulima wakati wa zoezi la usajili na kupelekea ugumu katika kuweka kumbukumbu za usajili, baadhi ya wakulima wamekuwa wakipeleka vitambulisho visivyo sawa na taarifa wanazojaza kwenye fomu. Aidha, idadi ya mikarafuu inayosajiliwa kuwa tofauti na ukubwa wa shamba wakati wa ukaguzi na kupelekea kutokuwa na takwimu sahihi za wakulima na mikarafuu.

4. Shirika linakabiliwa na ukosefu wa huduma za kibenki katika vituo vya mauzo ya karafuu. Pamoja na ukweli kwamba fedha nyingi zinatolewa kwa ajili ununuzi wa karafuu, wakulima wamekua hawako tayari kutumia huduma za kibenki kupokea malipo ya mauzo yao, hali inayohatarisha usalama wa maisha yao, maisha ya wafanyakazi pamoja na mali zao.

5. Kushuka kwa bei ya Karafuu katika soko la Dunia na kunapelekea Shirika kutouza karafuu zake kwa kipindi ambacho bei ipo chini na kusubiria hadi bei hiyo inapokua juu. Hali hii inapelekeka Shirika kuingia gharama za kuhifadhi Karafuu kwa muda mrefu ambako husababisha Karafuu kunywea na kupunguza uzito na thamani yake kwa kiasi kikubwa.

6. Kuchelewa kurejeshwa mikopo ya wakulima ni tatizo linalopelekea Shirika kutumia muda mwingi pamoja na gharama kubwa kufuatilia malipo ya mikopo hiyo.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Kwa kuzingatia umuhimu wa kuweka mazingira salama kwa wakulima na wafanyakazi wa Shirika, Kamati inashauri Serikali kupitia Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar - ZSTC kufanya malipo ya ununuzi wa Karafuu kupitia Benki kuwa ni suala la lazima na sio hiari. Aidha, kufanya malipo kwa njia ya benki kutaimarisha mzunguko wa fedha na kurahisisha ulipaji wa mikopo.

2. Kutokana na ushindani mkubwa wa soko kwa nchi nyengine zinazozalisha Karafuu, Kamati inaishauri Shirika la ZSTC lifanye kazi ya kufuatilia taarifa za uzalishaji karafuu katika nchi hizo ili kuweza kupanga mikakati itakayoliwezesha Shirika kuhimili ushindani. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kulitumia jina la Zanzibar kama alama ya kibiashara “brand” kwa bidhaa zinazozalishwa Zanzibar ikiwemo karafuu pamoja na bidhaa nyengine za viungo.

3. Kwa kuwa mikopo inayotolewa na Shirika ni kwa ajili ya Uchumaji wa karafuu na sio umiliki wa mashamba ya karafuu. Kamati inaishauri Shirika litafute utaratibu utakaowawezesha wafanyabiashara wanaokodi mashamba kupata mikopo hiyo, sambamba na kuweka utaratibu utakaohakikisha wanapatiwa mikopo na kurejesha kwa wakati.

4. Kamati imebaini kuwa licha ya Shirika la ZSTC kutumia kiwango kikubwa cha fedha kwa ajili ya ununuzi wa karafuu, mzunguuko wa fedha hizo hauonekani katika benki za ndani kwa mfano, msimu wa mwaka 2017 Shirika limetumia kiasi cha Tsh 112,972,773,250/- kwa ajili ya ununuzi wa karafuu. Kamati inalishauri Shirika lifanye utafiti iwapo fedha hizo zinaekezwa nje ya Zanzibar au zinabakishwa majumbani bila ya kuhifadhiwa benki, Utafiti juu ya fedha hizo utasaidia Serikali katika kupanga mipango yake ya maendeleo.

## KIWANDA CHA MAKONYO

Kamati ilifanya ziara katika kiwanda cha Makonyo kilichopo Pemba kwa lengo la kuona maendeleo pamoja na changamoto zinazokikabili kiwanda hicho na kutoa ushauri juu ya namna bora ya kukabiliana na changamoto hizo, ili kukisaidia kiwanda kujiendesha kwa faida na hatimae kusaidia katika uchumi wa nchi.

Kamati iliarifiwa kuwa Kiwanda hicho kinazalisha aina saba za mafuta ikiwemo Mafuta ya Makonyo, Mafuta ya Mchaichai, Mafuta ya Mdalasini, Mafuta ya Mrehani, Mafuta ya Mkaratusi Madawa, Mafuta ya Manukato na Mafuta ya Mkarafuu. Aidha, Kamati iliarifiwa kwamba Kiwanda kina jumla ya wafanyakazi 32 wa kudumu wakiwemo wanaume 18 na wanawake 14 sambamba na wafanyakazi wa muda ambao idadi yao inategemea aina ya kazi zilizopo.

## CHANGAMOTO ZA KIWANDA CHA MAKONYO

1. Uchakavu wa mashine zinazotumika katika kiwanda ambazo hazijafanyiwa matengenezo makubwa kwa muda mrefu tokea kuanzishwa kwa kiwanda hicho mnamo mwaka 1982. Uchakavu huo hupelekea kiwanda kufanya kazi kwa siku 42 hadi 60 badala ya siku 200 ambazo kiwanda kinachopaswa kufanya kazi kwa mwaka na hupelekea kuendeshwa kwa hasara. *(Angalia kiambatanisho namba 2)*.
2. Utumiaji wa mbinu za kizamani za uzalishaji na uendeshaji biashara pamoja na kuwepo kwa tabia ya wizi kwa baadhi ya wafanyakazi wa muda wanaofanyakazi kiwandani hapo , kunapelekea kiwanda kushindwa kuzalisha kwa kiwango kikubwa, na hivyo bidhaa chache zinazozalishwa kutokidhi mahitaji ya soko na kurejesha nyuma maendeleo ya kiwanda.

3. Uvamizi wa wananchi katika shamba la MTAKATA linalotumiwa na kiwanda kwa ajili ya kuzalisha miti ya mafuta. Kamati imearifiwa kati ya eneo lote la shamba lenye ukubwa wa hekta 230 ambalo kiwanda inalilipia kodi ya ardhi (lease) takriban hekta 120 zimeshavamiwa na wananchi kwa ajili ya shughuli za kilimo.

4. Maradhi yanayoyakabili baadhi ya mimea inayotumika katika kuzalisha mafuta kama vile mchaichai pamoja na ukame katika shamba la MTAKATA unaosababishwa na uhaba wa mvua ambao hupelekea kutonawiri vizuri kwa mimea, na hivyo kufa kwa baadhi ya mimea katika shamba hilo.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Ili kukiwezesha kiwanda kuwa na ufanisi, Kamati inaushauri uongozi wa Kiwanda uangalie mbinu mpya za kukiendesha kiwanda hicho ikiwa ni pamoja na kuangalia uwezekano wa kukiendesha kwa ubia (Joint Venture) kwa kushirikiana na kampuni binafsi zenye uzowefu. Aidha, Kamati inashauri kiwanda kifanye kazi kwa kujitegemea badala ya kufanya kazi chini ya mwamvuli wa Shirika la Taifa la Biashara (ZSTC) ambapo ni vigumu kupima ufanisi halisi wa kiwanda kutokana na kubebwa na Shirika kwa baadhi ya gharama.

2. Kamati inaushauri uongozi wa Kiwanda kuomba hati ya umiliki wa shamba la MTAKATA ambalo Kiwanda inalilipia Kodi ya Ardhi "lease" ili kuweza kudhibiti uvamizi wa wananchi.

3. Kamati inautaka uongozi wa Kiwanda kuendeleza juhudi za kupunguza hasara za uzalishaji kwa kuhakikisha kiwanda kinazalisha kwa faida. Ili kupata ufanisi katika uendeshaji wa Kiwanda hicho Kamati inaushauri uongozi wa Kiwanda kufanya uchambuzi wa kina juu ya mahitaji halisi ya kiwanda sambamba na kuweka mikakati mipya na mbinu za kisasa katika uendeshaji wa kiwanda hicho.

4. Kamati inaushauri uongozi wa Kiwanda kuweka mikakati imara ya kudhibiti wizi ambao unaathiri shughuli za uzalishaji katika kiwanda hicho dhidi ya watakao bainika kufanya vitendo hivyo.

## HOSPITALI YA ABDALLAH MZEE PEMBA

Kamati katika kufuatilia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali, ilipokea taarifa ya uendelezaji na utunzaji wa Hospitali ya Abdallah Mzee - Pemba, taarifa ambayo ilijumuisha utekelezaji wa shughuli za hospitali ikiwemo mafanikio na changamoto mbali mbali zinazoikabili hospitali hiyo.

## CHANGAMOTO ZA HOSPITALI

1. Uchache wa wafanyakazi katika hospitali ambapo kwa sasa kuna wafanyakazi 196 badala ya wafanyakazi 500 wanaohitajika, hali inayozorotesha utendaji kazi wa hospitali hiyo. Mahitaji hayo ya wafanyakazi yanajumuisha madaktari wa macho, madaktari wa upasuaji wa meno, madaktari wa mionzi (radiologist), wauguzi na fundi wa mitambo.
2. Kutokutumika kwa baadhi ya vifaa tiba ndani ya hospitali kutokana na kutokamilika kwake au kukosekana kwa wataalamu wa kuvitumia hali inayopelekea vifaa hivyo

kubakia tu katika maabara bila ya matumizi yoyote. Kwa mfano kutokufanyika kwa vipimo vya “Histopathology, Haematology, EEG, ECHO na Endoscopy katika maabara ni kutokana na kukosa utaalamu wa kuvitumia vifaa hivyo au “reagents”.

3. Kutokuwepo kwa mazingira rafiki kwa wafanyakazi ikiwa ni pamoja na kukosekana kwa nyumba za madaktari katika eneo la hospitali, kunakopunguza ufanisi wa huduma zinazotolewa.
4. Hospitali haina mfumo wa kisasa wa ukusanyaji wa takwimu mbali mbali za wagonjwa hali inayopelekea kutokupata kwa mahitaji yanayostahiki katika takwimu hizo.
5. Kutokupatikana kwa fedha za bajeti zilizotengwa kwa ajili ya hospitali kwa ukamilifu hali inayozorotesha shughuli za uwendeshaji za hospitali. ( *Angalia kiambatanisho namba 3 kuhusiana na Bajeti ya Hospitali)*

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaishauri Wizara ya Afya kuharakisha upatikanaji wa wafanyakazi katika hospitali ili waweze kuenda sambamba na mahitaji halisi yaliyopo hospitalini hapo. Aidha, Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha kuwa vifaa vilivyopo vinatumika ipasavyo kwani kwa sasa kuna baadhi ya mashine kama vile katika sehemu ya maabara hazitumiki na kukosekana kwa vipimo vya “EEG”, “ECHO” na “Endoscopy” kunakotokana na kukosekana kwa wataalamu.
2. Kamati inaishauri Wizara kujenga nyumba za wafanyakazi karibu na eneo la hospitali hiyo, ili kuondoa usumbufu kwa madaktari na wauguzi wanaoishi Chake chake ambao huletwa na kurejeshwa kwa gari kila siku, ili kupunguza gharama kubwa za mafuta ambazo zingeweza kufidia katika shughuli nyengine za hospitali.
3. Kamati inaishauri Wizara kuzingatia utekelezaji wa ukusanyaji wa takwimu kwa njia za kisasa katika hospitali hiyo, ili kurahisisha upatikanaji wa takwimu za wagonjwa kwa haraka zaidi na pia kuhakikisha kuwa zinatuzwa katika hali ya ubora.
4. Ili kuhakikisha hospitali inamudu gharama za uendeshaji na utunzaji, Kamati inaishauri Wizara ya Afya kuipatia hospitali hiyo fedha zake kama zilivyoizinishwa katika Bajeti.

## MRADI WA UJENZI WA SKULI ZA SEKONDARI ZA KISASA - PEMBA

## (SKULI YA SEKONDARI MADUNGU NA WAWI)

Kamati ilipokea taarifa ya ujenzi wa skuli za kisasa kwa upande wa Pemba ambao upo chini ya Mradi wa ZABEIP uliogharimu dola za kimarekani 42,000,000/= ambazo ni mkopo kutoka Benki

ya Dunia. Aidha Kamati ilifanya ziara ya kukagua skuli ya Madungu na Wawi ambazo zimejengwa kupitia mradi huo ili kuona ubora wa skuli hizo.

**CHANGAMOTO ZA SKULI YA SEKONDARI MADUNGU NA SKULI YA WAWI**

1. Kukosa ubora uliotarajiwa kwa skuli ya Madungu na skuli ya Wawi kulikopelekea kuvuja kwa baadhi ya maeneo ya skuli hizo kama vile madarasa, vyumba vya komputa na maabara pamoja na kufanya nyufa, hali inayohatarisha usalama wa wanafunzi, walimu na vifaa vilivyopo katika skuli hizo na kuibebesha Serikali gharama.(*Angalia kiambatanisho namba 4)*

2. Ufinyu na ubovu wa miundombinu ya umeme na vyoo kwa upande wa skuli ya Madungu ambayo kimsingi haikidhi haja kwa usalama wa watumiaji wa skuli hiyo. Aidha, kwa upande wa Skuli ya Wawi sakafu yake hairidhishi kutokana na rangi iliyotumika kutokuwa katika ubora.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

1. Ili kuhakikisha ubora wa skuli zinazojengwa, Kamati inaishauri Wizara ya Elimu na mafunzo ya Amali, kuchagua kampuni zenye wakandarasi wenye uzoefu na uweledi mkubwa wa kuipitia michoro na kubaini mapungufu yoyote ambayo yatarekebishwa tokea hatua za mwanzo. Aidha, Kamati inashauri Wizara waweke wasimamizi wenye utaalamu wa kutosha katika ujenzi ili kuweza kubaini kasoro.

2. Kamati inaishauri Wizara kuangalia na kuipitia vyema mikataba baina yao na makampuni zinazoshinda zabuni kwa lengo la kuifanya mikataba hiyo ikidhi haja na kuweza kuwawajibisha wazabuni hao pale kasoro zitakapojitokeza.

3. Kufuatia kasoro mbali mbali zinazojitokeza katika miradi inayofadhiliwa na washirika wa maendeleo, Kamati inaishauri Wizara kuwa na ushawishi mkubwa katika kuingia mikataba na wahisani hao, kwa kuweza kuainisha mahitaji ya miradi yao na hata kubadilishwa kwa maandiko ya mikataba pindi mikataba na michoro hiyo itakapobainika kuwa na kasoro.

4. Kamati inaishauri Wizara iandae mkakati mpya na wa muda mrefu utakaohakikisha kasoro zilizojitokeza katika utekelezaji wa miradi hazitojitokeza tena, na kuzingatia suala zima la kutekeleza miradi kwa kiwango cha ubora zaidi na kuhakikisha kuwa watendaji ambao wataenda kinyume na utaratibu wa kutekeleza miradi hiyo wanachukuliwa hatua za kisheria.

**WIZARA YA KILIMO, MALIASILI NA MIFUGO.**

Kamati ilipokea taarifa ya Utekelezaji wa Mradi wa Maendeleo ya Uvuvi na Hifadhi za Baharini, taarifa ya Programu ya Maendeleo ya Kilimo pamoja na kutembelea ghala la kuhifadhia chakula.

Kamati pia ilifanya kikao cha pamoja na Mamlaka ya Uwekezaji wa Ukuzaji wa Vitega Uchumi (ZIPA) na Wizara ya Kilimo, Maliasili na Mifugo kwa lengo la kujadili miradi ya sekta ya uvuvi iliyokwama utekelezaji wake.

Kupitia kikao cha pamoja, Kamati iliarifiwa na ZIPA kuwa kwa kipindi cha mwaka 2017/2018 kati ya miradi 18 iliyopitishwa, miradi 7 imepatiwa cheti cha uwekezaji, miradi 3 haijaendelezwa na miradi 8 haijapata ardhi na vibali vyengine. (*Angalia kiambatanisho namba 5)*

**CHANGAMOTO**

1. Wawekezaji kushindwa kufuata taratibu zilizowekwa katika uwekezaji kwa sekta husika. Ifahamike kuwa licha ya ZIPA kuwa ndio msimamizi wa uwekezaji lakini pia sekta husika ina majukumu yake katika kuhakikisha kuwa uwekezaji unazingatia Sheria na Masharti yaliyopo ambayo yanalinda utunzaji wa mazingira na rasilimali za baharini.

2. Ugumu wa upatikanaji wa ardhi kutokana na kukosekana kwa miongozo ya mipango miji na vijiji na taratibu za nchi kwa ajili ya uwekezaji husika, ambapo miongoni mwa mahitaji ya wawekezaji wa sekta ya uvuvi ni fukwe kwa ajili ya ujenzi wa gati na viwanda vya kusarifu mazao ya baharini.

3. Changamoto ya Sheria zinazohusiana na Sekta ya uvuvi kujikita zaid katika kuboresha utawala na uendeshaji wa sekta hiyo kuliko kuweka mazingira rafiki ya biashara, hali inayopelekea gharama ya uwekezaji katika sekta hii kuwa kubwa na kurudisha nyuma jitihada za wawekezaji.

4. Kuhusiana na mradi wa kuendeleza mazao baharini uliopo eneo la Beit Ras Mtoni unaojumuisha ujenzi wa kituo cha kutotolea vifaranga vya samaki, Kamati imebaini kuwa uendeshaji wa mradi huo unahitaji utaalamu mkubwa pamoja na ufuatiliaji wa karibu ili kuweza kutunza viumbe hao pamoja na vyakula wanavyotayarishiwa kwa ajili ya ukuaji wao.

5. Kupungua kwa uzalishaji wa baadhi ya mazao muhimu ya chakula nchini ikiwemo zao la mpunga hali inayopelekea kuendelea kutegemea kuagiza vyakula kutoka nje ya nchi kama vile mchele kutoka Vietnam, licha ya kuwepo kwa programu ya maendeleo ya umwagiliaji maji.

6. Kutokuwepo kwa ghala la kuhifadhia chakula Zanzibar kwa kipindi kirefu, hali inayohatarisha usalama wa chakula na lishe nchini.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaishauri ZIPA kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kuzifanyia kazi changamoto za kisheria na kuendelea kuwapatia elimu wawekezaji katika mchakato mzima wa uwekezaji nchini pamoja na taratibu zilizopo ili wawekezaji wapate uwelewa mpana wa taratibu zote kabla ya kufanya maamuzi ya uwekezaji.

2. Kwa kuwa imebainika kuwa, wawekezaji wengi wanahitaji maeneo ya fukwe, kuna haja ya Serikali kujipanga na kujizatiti kwa kuyawekea masharti ya kuyatumia maeneo hayo, ili iwapo muwekezaji atapatiwa sehemu aitumie kwa mujibu wa masharti na matakwa ya nchi.

3. Kwa kuwa mradi wa kuendeleza mazao baharini ni wa gharama kubwa (dola za kimarekani milioni 3.2) na unahitaji muda na umakini katika kuufanikisha, Kamati inaishauri Serikali kufikiria kueka mikakati madhubuti ya kutumia rasilimali ya bahari ambayo tayari tunayo katika kuzalisha na kuvuna samaki.

4. Kwa kuwa Kamati imebaini kuwa uzalishaji wa mazao ya chakula nchini umepungua, Kamati inaishauri Wizara kupitia mradi wake wa maendeleo ya kilimo kuendeela kutoa mafunzo ya kilimo bora cha mazao mbali mbali pamoja na kuwawezesha wakulima kutumia mbinu za kisasa ili uzalishaji uweze kuongezeka.

5. Kamati inaunga mkono jitihada za Wizara za kuendelea na ujenzi wa ghala la kuhifadhia chakula liliopo Malindi, ambalo kimsingi litasaidia kuwepo kwa usalama wa chakula nchini na kusaidia wakulima kupata soko la bidhaa zao. Kamati inaisisitiza Wizara kusimamia vyema ujenzi wa ghala hilo ili liwe katika kiwango kinachostahiki pamoja na kulitumia kwa malengo yaliyokusudiwa.

## MRADI WA JENGO LA TERMINAL 2

Kamati iliarifiwa kuwa ujenzi wa Jengo Jipya la Abiria la Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume umeanza utekelezaji wake tokea mwaka 2010 ambapo Mkataba wa Ujenzi huo ulikuwa Baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji na Kampuni ya Beijing Construction Engineering Group (BCEG) ya China uliotiwa saini mwaka 2009 ukigharimu jumla ya USD 70.4 milioni zilizotolewa na Benki ya Exim ya China kwa ajili ya ujenzi wa uwanja huo. Hata hivyo, kutokana na mabadiliko ya ujenzi ambayo yalitokana na kasoro zilizojitokeza, gharama za mradi huo zimeongezeka hadi kufikia USD 128.7 milioni.

## CHANGAMOTO YA MRADI WA JENGO LA TERMINAL 2

1. Kamati imebaini changamoto ya kimkataba iliyopo baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Kampuni ya ujenzi ya China (BCEG) ambapo katika kutekeleza mradi huo

kulitokea kasoro za kiutendaji zilizosababishwa na Kampuni ya BCEG zilizopelekea kusimama kwa shughuli za mradi na huku gharama za kasoro hizo kuendelea kubebwa na Serikali, jambo mbalo ni kuitia hasara Serikali na kuiongezea gharama zisizotarajiwa.

2. Kamati imeweza kubaini kuwa katika utekelezaji na uendeshaji wa miradi suala la muda ni la kuzingatiwa sana ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Kwa mujibu wa mkataba wa utekelezaji wa mradi huo ulitakiwa kukamilika mnamo mwezi Novemba 2017. Kutokana na kasoro zilizojitokeza ikiwemo sehemu ya maegesho ya ndege na Jengo jipya la abiria kuwa karibu kiasi cha mita 60 kutoka sehemu ya kurukia na kutua kwa ndege ambapo kutapelekea usumbufu wakati wa kuegesha kwa ndege kubwa, kuwepo kwa tofauti za miinuko baina ya jengo jipya na sehemu ya kuegeshea ndege iliyojengwa mkabala na jengo hilo na jengo kutokuwa na uwiano kufuatana na utaratibu wa sheria za Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga- ICAO, kumepelekea mradi kutomalizika kwa wakati na kulazimika kushughulikiwa kwa kasoro hizo.

3. Kamati imeweza kubaini kuwa Serikali imeingia gharama mpya za USD 58.3 milioni zilizokuwa hazimo katika mradi kutokana na madiliko ya ujenzi yaliyopendekezwa na mshauri elekezi kupitia kampuni ya ADPi.

4. Kutowajibishwa kwa Kampuni ya BCEG ambayo ilisababisha kasoro mbali mbali katika mradi huo, pamoja na kutoathiriwa malipo yao kwa vile Serikali ilitakiwa kulipa Kampuni kwa kiwango walichokubaliana, ili hatimae Kampuni iendelee na Ujenzi.

5. Kamati imebaini kuwa licha ya mradi huo kugharimu fedha nyingi na muda mkubwa, hadi sasa haujakamilika na haujulikani lini utakamilika. Aidha, Serikali inapaswa kulipa mkopo wa mradi huo ifikapo mwaka 2019.

6. Kamati imebaini eneo lilotengwa kwa ajili ya abiria wanaowasili ni dogo sana kiasi cha kutomudu kupokea abiria wengi iwapo ndege zitawasili kwa pamoja. Aidha, Kamati imearifiwa ifikapo mwaka 2023, uwanja utakuwa ushazidiwa uwezo kiasi cha kutoweza kuhudumia ndege tatu kubwa kwa wakati mmoja.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaishauri Serikali kuwa na wataalamu wa kutosha wa kupitia na kufahamu mikabata ya miradi kabla haijaikubali miradi husika ili kuepusha kuzorota kwa miradi hiyo pamoja na upotovu wa fedha za Serikali.

2. Kwa kuwa utekelezaji wa mradi huu umeigharimu Serikali na kupelekea kufanya matumizi ya ziada tofauti na makadirio ya awali, Kamati inaishauri Serikali kutoendelea kuchukua makampuni ambayo yanatia kasoro za utekelezaji wa mradi na pia Mamlaka zinazohusika kuchukua hatua za kinidhamu kwa yeyote aliyepelekea kasoro hizo na kutokukamika kwa mradi kwa muda uliopangwa.

3. Kamati inaishauri Serikali katika kutekeleza miradi yake kuzingatia mikakati ya muda mrefu zaidi wa kuweza kutumika na kunufaika na mradi husika. Kwani Kamati imebaini kuwa licha ya Mradi wa Terminal II kuanza kutekelezwa 2010, muda wa mradi huo kukidhi mahitaji hautokuwa mrefu sana kabla ya jengo kuzidiwa uwezo kwa kuwa mahitaji yanazidi kila siku na mradi haukuandaliwa kwa kuzingatia mahitaji ya muda mrefu.

4. Kutokana na ufinyu wa eneo lililotengwa kwa ajili ya abiria wanaowasili(arrival) Kamati inashauri eneo hilo liongezwe ukubwa kwa kuhamisha sehemu ya V.I.P iliyopo eneo hilo na badala yake kutumika kwa V.I.P ya juu.

5. Kamati inaishauri Serikali kuwa na uwazi katika utekelezaji wa Miradi yake hususan katika kuwapata wakandarasi na wasimamizi wenye sifa. Hii ni kutokana na kutokupata taarifa za uhakiki kuhusu msimamizi wa awali wa Jengo la Terminal II wakati Kamati ilipofanya ziara ya Kulitembelea.

## IDARA YA SERIKALI MTANDAO

Kamati ilifanya ziara ya kukagua utekelezaji wa Mradi wa Serikali Mtandao ambao upo chini ya Idara ya Serikali Mtandao kupitia Wizara ya Katiba na Sheria. Mradi huu unatekelezwa kama njia moja wapo ya utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya 2020 ya Zanzibar na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA). Mradi huu unatekelezwa kupitia Programu ya Usimamizi na Uendeshaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA). Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 programu hii iliidhinishiwa Jumla ya Tsh 10,658,144,200 kati ya hizo Tsh 283,144,200 ni mishahara na Tsh 325,000,000 ni matumizi mengineyo. Aidha, Tsh 10,500,000,000 zilidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya Mradi. Tsh 50,000,000 mchango wa SMZ na Tsh 10,000,000 Mchango wa Washirika wa Maendelo

Serikali ilibuni na kutekeleza Mradi wa Serikali Mtandao (e-Government) kwa Ushirikiano na Serikali ya watu wa China kupitia Mkopo nafuu wa Benki ya Exim. Mradi huu ulianzishwa kwa madhumuni ya kuimarisha utendaji na utoaji wa huduma za Serikali kwa kuziunganisha taasisi zote za Serikali kupitia Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano ya Habari pamoja na kuiunganisha Zanzibar kupitia Mkonga wa Kimataifa, pia kuviunganisha visiwa vya Pemba kupitia teknolojia isiyotumia waya ya (Micro wave link). Mradi huu pia ulihusisha uanzishaji wa Kituo Kikuu cha kuhifadhia Taarifa (National Data Centre) kilichopo Mazizini.

Kamati imebaini utekelezaji wa mradi huu bado haujaleta ufanisi uliotarajiwa kutokana na taasisi nyingi za Serikali kutounganishwa taarifa zao katika kituo cha Kuhifadhia taarifa “Data Center”. Aidha, huduma ya “internet” imekua ya kusuasua kwa baadhi ya taasisi zilizoungwa na Mkonga, ambapo baadhi ya taasisi hizo zinalazimika kutumia makampuni mengine binafsi katika kupata huduma hiyo, hivyo kupelekea kutofikia lengo la kupunguza gharama za matumizi ya Serikali kama ilivyotarajiwa. Sambamba na hayo, Kamati pia iliarifiwa kwamba Taasisi ambazo

zinatumia huduma ya internet kupitia Mkonga huo zinapatiwa huduma hiyo bila malipo, hali inayoweza kudhoofisha maendeleo ya mradi huo hasa ikizingatiwa kwamba, taasisi hizo kiutaratibu zinatakiwa kulipia huduma hiyo.

## CHANGAMOTO ZA MRADI

1. Bajeti ya Idara ni ndogo kiasi cha kutoiwezesha Idara kufanya kazi zake kwa ufanisi.
2. Bado taasisi nyingi za Serikali hazijaungwa na Kituo cha kuhifadhia taarifa "Data Center'', na kuendelea kuhifadhi na kubadilishana taarifa kwa mfumo wa kizamani bila ya kuwa na mfumo wa kielectroniki kunakopelekea kuchelewa au kupotea kwa baadhi ya taarifa iwapo kutakuwa na mazingira ya kuhama kutoka jengo moja la Ofisi na kuelekea sehemu nyengine au kunapotokea majanga yoyote yasiyotarajiwa.
3. Tatizo la kukatika kwa huduma ya mtandao mara kwa mara inayosababishwa na mfumo wa Mkonga uliowekwa.
4. Huduma ya mkonga bado haijafika katika sehemu za vijijini na kwa sasa sehemu kubwa ya mkonga ipo maeneo ya mjini.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Kwakuwa, bado kuna taasisi nyingi za Serikali hazijaanza kutumia kituo cha kuhifadhia taarifa "Data Center", Kamati inaishauri Serikali ihakikishe taasisi hizo zinatumia kituo hicho kwa kuweka kumbukumbu za taarifa zao ili kutimiza malengo ya kuanzishwa kituo hicho na kuweza kutunza kumbukumbu za Serikali kwa uhakika na kwa muda mrefu zaidi bila ya kupotea na kuharibika.
2. Kwa kuwa Idara inakabiliwa na changamoto ya Bajeti na ili kuiwezesha kujiendesha kwa ufanisi, Kamati inashauri Serikali kuandaa utaratibu utakaoelekeza taasisi ambazo zimeunganishwa na kituo cha kuhifadhia taarifa "Data Center" na ambazo pia zinapata huduma ya "Internent" namna ya kulipia gharama ya huduma hizo.
3. Katika kuanzisha mfumo wa E-tax ambao ni sehemu ya Mradi wa Serikali Mtandao

   (e – Government), Kamati inashauri mfumo huo uanze kutumika kwa taasisi za Serikali badala ya taasisi za binafsi pekee. Hii itasaidia kuhamasisha wafanyabiashara kuutumia mfumo huo na kuzifahamu changamoto zake za utekelezaji mapema kabla haujaanza kutumika kwa sekta binafsi.
4. Idara ifanye tathmini ili ijuwe namna inavyoweza kujiendesha kibiashara kwa kuzitambua fursa za kibishara zinazoweza kupatikana kupitia huduma za Mkonga, hususan katika maeneo mapya ya uekezaji kama vile katika eneo la Mradi wa Nyumba za Makaazi Fumba pamoja na Uwanja wa Ndege "Terminal II". Kamati inaisisitiza Idara kuwa na

mipango mizuri ya baade “Future Plans” katika kuendesha Mradi na kuufanya uwe endelevu.

5. Katika jitihada za kuendeleza elimu kama kipaumbele cha Taifa, Kamati inashauri Serikali izingatie uwezekano wa kuiunganisha Wizara ya Elimu na mkonga kwa kuwapatia huduma ya Intaneti maskulini ambayo pia itawarahisishia wanafunzi katika kujisomea na kujipatia maarifa mapya.
6. Katika utekelezaji wa awamu ya pili ya Mradi, Kamati inaishauri Idara izingatie kuwashirikisha wadau katika hatua mbali mbali sambamba na kusikiliza maoni yao, hususan wadau wa sekta binafsi.

## MRADI WA UJENZI WA BANDARI YA MPIGA DURI

Kamati imeelezwa kuwa mradi huu unatarajiwa kujengwa katika eneo la Mpigaduri Maruhubi Mjini Zanzibar kwa mfumo wa ubia kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Kampuni ya China Harbor Engineering Company Ltd (CHEC) na kugharimu jumla ya USD 231,400,000, ambapo kati ya fedha hizo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itatoa jumla ya USD 200,000,000 kupitia mkopo wa Benki ya China – Exim Bank na Kampuni ya China Harbor Engineering Company Ltd itatoa jumla ya USD 31,400,000. Mkataba wa ujenzi huo umetiwa saini mnamo mwaka 2014 kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Kampuni ya CHEC.

## CHANGAMOTO ZA MRADI WA UJENZI WA BANDARI YA MPIGA DURI

1. Kamati imebaini ujenzi wa Bandari hiyo upo katikati ya Mji kiasi cha kutoweza kutatua changamoto ya msongomano mkubwa wa watu katika eneo finyu la Bandari pindi mradi huo utakapomaliza kujengwa na kuanza kutumika.
2. Kamati imeweza kubaini kuwa licha ya baadhi ya hatua za mradi kuanza kukamilika kama vile upembuzi yakinifu, kusainiwa kwa mkataba wa makubaliano ya Ubia, kusainiwa kwa mkataba wa ujenzi, kuna hatua muhimu ya rasimu ya mkataba wa fedha “Draft Financing Agreement” ambayo inatakiwa kupitiwa na kupatiwa maoni na Wizara ya Fedha ya SMT ambayo kukamilika kwake kutapelekea mkataba halisi kuweza kutiwa saini na kuweza kuendelea na hatua za mkataba wa mkopo ambao ni muhimu sana katika kupelekea kupatikana kwa fedha na hatimae mradi kuanza kutekelezwa. Hadi Kamati inapokea taarifa ya utekelazaji wa mradi huu, mapitio ya rasimu ya mkataba wa mkopo bado hayajafanyika.
3. Kamati imebaini kuwa katika eneo la ujenzi wa bandari ndani yake kuna makumbusho ambayo yameachwa bila ya kushughulikiwa, ambapo ujenzi wa bandari utakapoendelea ni

dhahiri kuwa makumbusho hayo hayatoendelezwa au yataathiriwa kwa vile yapo ndani ya eneo la ujenzi na kupelekea kupoteza kumbukumbu muhimu za nchi yetu.

4. Kamati imebaini kuwa katika eneo la Mpigaduri kuna diko ambalo wavuvi hulitumia kwa kufanya shughuli zao za mnada na kuwapatia ajira vijana. Hivyo, Kuanza kwa ujenzi wa bandari bila ya kuwajengea mazingira mbadala huenda kukaathiri shughuli zao na hivyo kuwapunguzia kipato.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kuhusiana na miradi ambayo upatikanaji wake wa fedha unategemea kutiwa saini kwa mikataba na Wizara ya fedha ya SMT, Kamati inashauri katika miradi ya aina hiyo, Wizara ya fedha ya SMZ kufanya mawasiliano na ufuatiliaji wa karibu ili kuhakikisha kuwa hatua zinakamilika kwa haraka na kuiwezesha miradi hiyo kuanza kutekelezwa.
2. Kamati inaishauri Serikali katika kutekeleza miradi mipya ifanye mazingatio ya maeneo kihistoria yanayohitaji kuhifadhiwa kama makumbusho, ili yaweze kubakia katika hali nzuri na kuiingizia mapato Serikali.
3. Kamati inaishauri Serikali wakati wa kuendeleza miradi yake izingatie vijana ambao wamejiajiri katika maeneo hayo, ili miradi hiyo isiwe sababu ya kuzuia ajira za vijana hao.

**WIZARA YA ARDHI MAJI NISHATI NA MAZINGIRA.**

Kamati kwa kuzingatia umuhimu wa Wizara hii, kutokana na mambo ya msingi ambayo inayasimamia, ikiwa ni pamoja na suala la mali ghafi ya mafuta ambayo kwa sasa Zanzibar ipo katika hatua za utafiti kuwa na mchango mkubwa katika kuendesha shughuli mbali mbali za maendeleo na pia kuchangia kiasi kikubwa cha kodi.

Kamati ya Bajeti iliamua kuchagua eneo mahsusi la mafuta ambalo athari zake ni kubwa kiuchumi. Kamati ilikutana na Mamlaka ya ZURA kwa ajili ya kujadili masuala yanayohusiana na mafuta Zanzibar pamoja na kukagua eneo la Mangapwani lililotengwa kwa ajili ya shughuli za mafuta na gesi. Aidha, kwa lengo la kupata uelewa zaidi na kuweza kuishauri vyema Serikali juu ya suala la mafuta, Kamati ilifanya ziara katika Mamlaka ya Udhibiti wa Maji na Nishati EWURA pamoja na Taasisi ya Uwakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa pamoja **(PBPA)** Tanzania Bara.

**ENEO LA KUHIFADHIA MAFUTA NA GESI NA UJENZI WA BANDARI UKANDA WA MANGAPWANI -BUMBWINI.**

Kamati ya Bajeti ilipata fursa ya kulitembelea eneo lililotengwa kwa ajili ya shughuli za kuhifadhi mafuta na gesi, bandari ya kuhudumia upakizi na ushushaji wa mafuta na gesi

pamoja na bohari ya kuhifadhia zana na vifaa vya mafuta kwa Zanzibar lililoko katika ukanda wa Pwani ya Bumbwini lenye ukubwa wa takriban hekta 380. Kamati iliarifiwa kuwa, maamuzi ya kutenga eneo hilo yalitokana na matarajio ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar juu ya kukua na kuongezeka kwa shughuli za matumizi ya mafuta na gesi.

**CHANGAMOTO**

1. Kutokukamilika kwa zoezi la kupima, licha ya eneo hilo kutengwa kwa ajili ya matumizi hayo tokea mwaka 1995.

2. Kutokuwepo kwa miundo mbinu rafiki na ya msingi ikiwa ni pamoja na barabara ya ndani ya kufikia eneo hilo na maji ambayo kiujumla ni vitu vya msingi katika biashara na shughuli za mafuta.

3. Kuwepo kwa maakaazi ya watu katika eneo hilo ambalo wanalitumia kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii, kiasi cha kuibua hofu kwa wakaazi wa maeneo hayo kuhusu hatma yao iwapo watahamishwa.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kutokana na kutokukamilika kwa zoezi la kulipima eneo la Mangapwani ambalo limetengwa kwa ajili ya matumizi ya shughuli za mafuta na gesi, na kwa kuwa Kamati imearifiwa kuwa, fedha kwa ajili ya upimaji wa eneo hilo zimeshaidhinishwa, Kamati inasisitiza Kamisheni ya Ardhi na Idara ya Upimaji zifanye haraka zoezi la kulipima eneo hilo, ili kuepusha uvamizi wa wananchi katika eneo hilo.

2. Kutokana na maendeleo ya teknolojia na kukuwa kwa kasi sekta ya Nishati ulimwenguni, Kamati inaishauri ZIPA kupitia Kamisheni ya Ardhi kutafuta mshauri elekezi juu ya namna bora zaidi ya kulipanga eneo hilo kwa kuzingatia mahitaji makubwa ya miaka ya usoni ya eneo la Mangapwani ambalo kwa sasa linaonekana linakidhi haja na ni kubwa kutokana na mahitaji na matumizi ya shughuli za mafuta kwa ujumla.

3. Kwa kuwa Serikali kupitia Mamlaka ya **ZURA** imeshaanza kutumia mfumo wa uwagizaji wa mafuta kwa pamoja yaani “BPS”, na kutokana na changamoto ya kuwa na sehemu ya kuhifadhia mafuta yenye uwezo mdogo kulinganisha na mahitaji ya kuufanya mfumo wa BPS kuleta faida zinazokusudiwa, Kamati inashauri kujengwa kwa “depot” mpya, kubwa na ya kisasa ambayo itahimili kuhifadhi mafuta mengi zaidi yanayolingana na mahitaji ya mfumo wa BPS.

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI (ZURA)**

Mamlaka hii imeundwa kwa Sheria namba 7 ya mwaka 2013 kwa lengo la kuleta ufanisi katika huduma za umeme, mafuta, gesi asilia na nishati nyengine yoyote ambayo itakua inazalisha umeme na kuhakikisha watumiaji wa nishati hizo wanapata huduma zinazostahili na

wafanyabiashara wanapata faida halali kutokana na biashara zao ili kuweza kuleta faida za kiuchumi na kijamii.

Kwa mwaka wa Fedha 2017/2018, miongoni mwa majukumu waliyojipangia Mamlaka ni pamoja na kukamilisha kanuni za ujenzi wa bohari na kuanzisha mfumo mpya wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja (Bulk Procurement System).

Itakumbukwa kwamba Serikali imeanza kutumia mfumo wa uagiziaji mafuta kwa pamoja (BPS) kwa lengo la kuongeza ubora, kuwa na udhibiti pamoja na kupunguza gharama za bidhaa hiyo. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa kutokana na changamoto mbali mbal zilizojitokeza, mfumo huo hauwezi kufikia malengo yaliyokusudiwa kwa sasa, na hauwezi kutekelezeka kwa ufanisi.

## CHANGAMOTO ZA MAMLAKA YA ZURA

1. **Ufinyu wa sehemu ya kuhifadhi mafuta (Storage Facilites):** mfumo wa Uagiziaji wa mafuta kwa pamoja BPS unahusisha uagizaji wa mafuta kwa kiwango kikubwa kwa kampuni ambayo imeshinda zabuni ya kuleta mafuta na kusambaza kwa makampuni ya ndani, ili kupata faida za kiuchumi. Kampuni ambayo inashinda zabuni ya kuleta mafuta hulazimika kuleta mafuta kwa kiwango kikubwa kwa kutumia meli kubwa, hata hivyo kutokana na kutokuwepo kwa eneo la kutosha la kuhifadhia mafuta katika maeneo ya bohari za Mtoni, Kampuni inayoshinda zabuni haiwezi kuagiza mafuta kwa kiwango kikubwa na hivyo hulazimika kuchukua mafuta kidogo katika Bandari ya Dar es Salaam kinyume na makubaliano ya kuagiza mafuta hayo kutoka nje.

2. **Kina Kidogo cha Maji katika eneo la Bohari ya Mtoni**: kutokidhi haja kwa hali ya bandari ya Mtoni kutokana na kina cha maji katika eneo hilo kuwa kidogo kwa meli kubwa kufunga gati. Uwezo wa bandari ya Mtoni ni kwa meli zisizozidi tani 3,500 na kwa upande wa Pemba ni meli zisizozidi tani 600, wakati hali halisi ya mahitaji ni kati ya tani 8,000 hadi tani 10,000. Suala hili linapelekea mletaji mafuta kushindwa kuleta mafuta moja kwa moja kutoka katika soko la dunia na badala yake hulazimika kuchukua mafuta kutoka nchini Kenya au kwenye mfumo wa BPS ya Dar es Salaam wakati gharama alizoweka ni kutoka katika soko la dunia.

3. **Miundombinu hafifu ya kushushia mafuta:** Miundombinu iliyopo sasa ya kushushia mafuta ni ya zamani na hairuhusu kushusha mafuta kwa kiwango kikubwa na kwa haraka hususan kwa meli kubwa, hivyo huongeza gharama na kuufanya mfumo wa BPS kuwa mgumu kutekelezeka kwa kutumia miundombinu iliyopo.

4. **Uchelewaji  wa Meli ya Mafuta**: mletaji wa mafuta huchelewa kuleta mafuta kwa wakti hali ambayo imekuwa ikisababisha upungufu wa mafuta mara kwa mara na kuleta usumbufu mkubwa katika shughuli za kijamii na kiuchumi.

5. **Kukosekana kwa Jengo la Ofisi ya Mamlaka:** Mamlaka ya ZURA inatumia majengo ya kukodi kwa shughuli za ofisi Unguja na Pemba. Kwa upande wa Pemba Mamlaka imekodi jengo la mtu binafsi kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi,Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto na  Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, kiasi cha kuinyima Mamlaka kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kutokana na ufinyu wa nafasi.

6. **Kutokuwepo ushindani katika biashara ya mafuta kwa upande wa Pemba**: Kuwepo kwa msambazaji mmoja wa mafuta kwa jumla pamoja na vituo vichache vya kuuzia mafuta kwa upande wa Pemba kunapunguza ushindani wa kibiashara na kunapelekea kuwepo biashara ya mafuta kwa njia za magendo.

7. **Kukosekana kwa kifaa maalum cha kupimia mafuta“Flow meter”**:  kutokuwepo kwa kifaa hicho katika Bohari za kuhifadhia mafuta (depot) kwa upande wa Unguja na Pemba kutokana na miundombinu iliyopo, hali inayoweza kupelekea udanganyifu katika upimaji wa mafuta na ulipaji kodi kwa ujumla.

8. **Kukosekana kwa mkataba baina ya ZURA na Makampuni ya uagizaji mafuta:** Kutokana na maamuzi ya Serikali ya kusitisha kwa muda mfumo wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja (BPS) na kuyaruhusu makampuni binafsi kuagiza mafuta, Kamati imebaini kutokuwepo kwa mkataba baina ya ZURA na makampuni hayo unaoweka masharti ya uagizaji mafuta  katika utaratibu  huo wa mpito.

9. **Uzoefu Mdogo wa Mamlaka katika Masuala ya Mafuta**: Mamlaka inakabiliwa na changamoto ya uzoefu katika masuala ya mafuta hususan katika mfumo mpya wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja (Bulk Procurement System), hali inayopelekea kutofikiwa kwa malengo halisi ya kuanzishwa kwa mfumo huo.

## MAONI NA USHAURI  WA KAMATI

1. Kwa kuwa Kamati imejiridhisha kwamba, mfumo wa BPS kwa sasa hauwezi kutekelezeka na kuleta faida kutokana na changamoto zilizopo. Kamati inaishauri Serikali kushughulikia suala la ujenzi wa Bandari mpya ya mafuta na Kujenga bohari yenye uwezo wa kuhifadhi mafuta mengi kabla ya kuanza kutumia mfumo huo. Kamati inashauri hivyo kutokana na hali ya kuadimika kwa mafuta inayojitokeza mara kwa mara ambayo kimsingi inaikosesha mapato mengi Serikali na kuhatarisha usalama wa nchi na vyombo na kuchochea kuwepo kwa mafuta ya magendo. Aidha, iwapo Serikali itaamua kuendelea

na mfumo wa BPS, Kamati inaishauri Mamlaka ya ZURA kuangalia uwezekano wa kutumia bohari “depot” zilizopo Bandari ya Mtwara ili kuepuka kuadimika kwa mafuta kunakotokea mara kwa mara.

2. Kamati inaishauri Mamlaka kutafuta hati miliki ya kiwanja kilichopo Pemba na kuanza utaratibu wa kuomba fedha kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Mamlaka.

3. Kamati inaishauri Mamlaka ya ZURA kufikiria namna ya kuwa na wasambazaji wengi wa mafuta tofauti na sasa ambapo kuna msambazaji mmoja tu kwa upande wa Pemba (GAPCO), kwa lengo la kuleta ushindani zaidi katika soko la mafuta na kupunguza wimbi la mafuta ya magendo ambayo yanaipotezea Serikali mapato kwa kiasi kikubwa. Aidha, Kamati inaishauri Mamlaka kwa kushirikiana na Bodi ya Mapato kutoa elimu zaidi kwa wananchi juu ya athari za uuzaji wa mafuta kwa njia za magendo.

4. Kwa kuwa Serikali ina mipango ya kujenga bohari mpya ya kuhifadhia mafuta “depot” katika eneo la ukanda wa mafuta-Bumbwini-Mangapwani, Kamati inaishauri ZURA na Serikali kwa ujumla, kuyashirikisha makampuni binafsi katika ujenzi wa “depot” hiyo na kuhakikisha uwepo wa miundombinu ya kisasa ambayo ni pamoja na kifaa maalum cha kupimia mafuta (Flow meter), ili kuhakikisha ufanisi wa hali ya juu katika bohari hiyo. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kutenga eneo jengine kwa upande wa Pemba kwa ajili ya bohari mpya na ya kisasa katika siku za usoni kama ilivyo kwa Unguja.

5. Kamati inaishauri Mamlaka ya ZURA kufunga mkataba na makampuni binafsi ya uletaji wa mafuta kwa kipindi cha mpito kwa lengo la udhibiti bora wa mfumo huo, kumlinda mteja na kuepusha kuadimika kwa bidhaa ya mafuta.

6. Kutokana na upya wa Mamlaka ya ZURA katika usimamizi wa shughuli za mafuta ambao unapelekea changamoto katika kutekeleza majukumu yake, Kamati inaishauri Mamlaka kuwajengea uwezo watendaji wake ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

## MAMLAKA YA UDHIBITI WA MAJI NA NISHATI-EWURA

Kamati katika kulipa uzito wa kipekee suala la malighafi ya mafuta kiuchumi, ilifanya ziara katika Mamlaka ya Udhibiti wa Maji na Nishati Tanzania Bara, ambayo kimsingi ina majukumu yanayolingana na yale ya **ZURA** kwa upande wa Zanzibar. Ziara hii ilikua na lengo la kuufahamu zaidi mfumo mpya wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja (BPS) ambao umeanza kutumika Zanzibar pamoja na changamoto zake. Pamoja na mambo mengine, ZURA inaweza kuyazingatia mambo yafuatayo kama ushauri.

1. Katika kulinda haki ya mtumiaji wa mafuta, kuna haja kwa **ZURA** kuanzisha mfumo wa kielektroniki kupitia simu ya mkononi ambao utamuwezesha mteja kuweza kutambua bei halisi ya mafuta kama utaratibu huo unavyotumiwa na EWURA. Hatua hii itasaidia kudhibiti ulanguzi na upandishaji holela wa bei za mafuta hususan kipindi ambacho mafuta yanaadimika.

2. Kamati imebaini kuwa EWURA kwa upande wa Tanzania Bara haina jukumu la moja kwa moja la kuagiza mafuta kwa mfumo wa BPS kama ilivyo ZURA kwa Zanzibar, na badala yake jukumu hilo linafanywa na Wakala wa Serikali wa Uwagizaji wa Mafuta kwa Mfumo wa Pamoja (PBPA). Aidha, Kamati inashauri Serikali kwa siku za usoni kuanzisha wakala wa Serikali ambae atakua na mamlaka ya kusimamia zoezi zima na kuendesha zabuni na kuagiza mafuta kwa mfumo wa BPS.

**3.** Kamati imejifunza kuwa ili Zanzibar ifaidike na mfumo wa **"BPS"** ambao umeshaanza kutumika kwa sasa ni vyema kukawepo sehemu ya kuhifadhia mafuta **"Depot"** yenye uwezo wa kuhifadhi mafuta kwa wingi zaidi, kulinganisha na ***"Depot"*** ndogo inayotumika kwa sasa, ambayo kwa namna inavyotumika haiwezeshi kufikia malengo ya mfumo huo wa kupata bidhaa bora ya mafuta na kwa bei nafuu.

## WAKALA WA UAGIZAJI WA MAFUTA KWA PAMOJA (PETROLEUM BULK PROCUREMENT AGENCY)

Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi ilipata fursa ya kukutana na Wakala wa Serikali wa Uwagizaji wa Mafuta kwa Pamoja kwa upande wa Tanzania Bara (PBPA) na kubadilishana uzoefu wao na wajumbe wa Kamati. Pamoja na mambo mengine ZURA inaweza kuyazingatia masuala yafuatayo kama ushauri wa Kamati katika utekelezaji wa mfumo wake wa uagizaji wa mafuta kwa jumla.

1. Kamati inashauri kuwepo na utaratibu maalum wa Mamlaka ya **ZURA** kushiriki katika zabuni zinazoendeshwa na kusimamiwa na **PBPA** kwa lengo la kujifunza na kubadilishana uzoefu juu ya namna gani zabuni hizo zinaendeshwa, kutokanana na ukweli kuwa, **PBPA** wana uzoefu zaidi juu ya zabuni hizo kulinganisha na Mamlaka ya ZURA katika suala la BPS.

2. Kamati imebaini kuwa, kumekuwa na udanganyifu kwa baadhi ya makampuni kudandia meli zinazoleta mafuta Tanzania Bara kwa gharama nafuu zaidi kulinganisha na ile wanayowasilisha kwa Mamlaka ya ZURA wakati wa zabuni na kupelekea makampuni hayo kupata faida kubwa. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Kamati inaishauri ZURA kuweka usimamizi madhubuti utakaohakikisha

kuwa kampuni inayoshinda zabuni inatimiza masharti yote ya kimkataba kama ilivyoanishwa katika nyaraka zilizotumika katika zabuni ikiwa ni pamoja na sehemu ya kwenda kuchukulia mafuta na meli itakayotumika. Aidha, ZURA wahakikishe wanapata takwimu sahihi kwa makampuni ya usambazaji mafuta juu ya hakiba na mahitaji ya mafuta ili kuepusha kuadimika kwa mafuta.

## MAMLAKA YA UVUVI WA BAHARI KUU

Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu ilianzishwa chini ya Sheria ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu namba 1 ya mwaka 1988 (The Deeep Sea Fishing Authority Act, No. 1 of 1998), iliyopitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata hivyo, hadi sasa Sheria hiyo bado haijaridhiwa na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

Pamoja na kutoridhiwa huko, Mamlaka ilianza kazi rasmi katika mwaka wa fedha 2009/2010 kwa mfumo wa makubaliano ya mpito (Interim Arrangement) kwa makubaliano baina ya Wizara zenye mamlaka ya uvuvi za SMT na SMZ hadi upande wa Zanzibar utakaporidhia Sheria hiyo. Aidha, mapato yanayopatikana yanagaiwa baina Serikali mbili za SMT na SMZ na sehemu ya mapato hayo yanabakia Mamlaka kwa ajili ya shughuli za undeshaji.

Kamati inaipongeza Mamlaka kwa namna inavyofanya kazi licha ya changamoto kadhaa zinazotokana na kutokuwepo kwa Sheria itakayowapa nguvu ya kufanya maamuzi ya msingi ikiwemo suala la uajiri. Kamati imebaini kupungua kwa meli za uvuvi na kushuka kwa mapato ya Mamlaka kutokana na mabadiliko ya Kanuni yaliyofanywa kwa lengo la kuongeza mapato, badala yake yamepelekea kupungua kwa meli za uvuvi kutokana kutokuwepo kwa huduma na miundo mbinu ya uhakika ya kuzihudumia meli ikiwemo bandari ya uvuvi.

## CHANGAMOTO ZA MAMLAKA YA UVUVI WA BAHARI KUU

1. Kutoridhiwa kwa Sheria ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu namba 1 ya mwaka 1998 kwa upande wa Zanzibar (Baraza la Wawakilishi).

2. Mamlaka kutokuwa na wafanyakazi wake wa kudumu na badala yake kutumia wafanyakazi walioazimwa kutoka taasisi mbali mbali za SMT na SMZ, hivyo kuifanya Mamlaka hiyo kutokuwa na uwezo wa kuajiri yenyewe.

3. Maslahi madogo ya wafanyakazi hasa ukizingatia Kazi za Mamlaka hii ni ngumu na pia ni za hatari hususan kazi za doria “*patrol*” za bahari kuu.

4. Kukosekana kwa bandari maalum ya uvuvi iliyotengwa kwa ajili ya maegesho ya meli za uvuvi kwa upande wa Zanzibar na Tanzania Bara, ambapo bandari zilizopo ni kwa ajili ya abiria na mizigo.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

1. Licha ya ukweli kwamba Zanzibar na Tanzania kwa ujumla ina rasilimali kubwa ya bahari, Sekta ya Uvuvi wa Bahari Kuu bado haijatumika ipasavyo na kupelekea mapato ya Bahari Kuu kusuasua. Aidha, sehemu kubwa ya mapato hayo yanategemea zaidi meli za nje kupitia mauzo ya leseni pekee.

2. Kwa kuwa Serikali ya SMZ imekubali Mamlaka ianze kazi kwa makubaliano ya mpito (interim arrangement), ni vyema Sheria ikawasilishwa Barazani kwa ajili ya kuridhiwa au kama kuna changamoto katika Sheria hiyo kuzitolea maelezo ili Wajumbe wa Baraza waweze kufahamu na kuiwezesha Mamlaka kufanya kazi kwa mujibu wa Sheria.

3. Mamlaka iandae vipindi vya televesheni na redio vya kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu shughuli za Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu kwa ujumla na kuandaa makongamano kwa wanafunzi wa vyuo vikuu kwa lengo la kupata uelewa zaidi katika shughuli za uvuvi wa bahari kuu.

4. Kamati inazishauri Serikali ya SMT na SMZ kuzipitia upya Kanuni za Mamlaka na kuzifanyia kazi changamoto za utekelezaji wake, hasa kwa kuzingatia kwamba miongoni mwa sababu zilizopelekea kupungua kwa meli za uvuvi na mapato, ni mabadiliko ya Kanuni yaliyofanywa, ambayo yameweka masharti kwa meli za uvuvi kushusha samaki katika bandari za ndani licha ya kutokuwepo kwa miundombinu imara ya kuzihudumia meli hizo.

5. Serikali kupitia Mamlaka iwawezeshe wavuvi wazawa kwa kuwapatia mafunzo na zana za kisasa ili waweze kuvua katika bahari kuu.

6. Ili kuvutia waekezaji na kuhimili soko la ushindani, Kamati inaishauri Serikali itilie mkazo suala la kujenga bandari maalum kwa ajili ya meli za uvuvi na kuimarisha utoaji wa huduma zote za meli ikiwemo maegesho ya meli, kushusha samaki haraka, kuhifadhi samaki, kusafirisha, ukarabati, zana za uvuvi, usafi, na kuandaa vifungashio vya bidhaa zinazotokana na uvuvi ili kuweza kuzipa hadhi bidhaa zinazozalishwa nchini. Aidha, Kamati inaishauri Serikali iangalie namna ya kuweka vivutio yaani"incentives" ikiwemo suala zima la kuwaondoshea "Fuel Levy" na kutoa ruzuku "Subsidize" ya mafuta kwa ajili ya Meli za Uvuvi.

## WIZARA YA HABARI UTALII UTAMADUNI NA MICHEZO-MRADI WA UJENZI WA UWANJA WA MAO ZEDONG

Kamati ilifanya ziara ya kuukagua Mradi wa Ujenzi wa Uwanja wa Mao tarehe 16/11/2017. Mradi huu unagharamiwa kwa pamoja baina ya Serikali ya China na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kamati iliarifiwa kuwa Ujezi wake umeanza kutekelezwa rasmi mwezi Machi 2017. Gharama za Mradi zinagharamiwa na Serikali ya China ambazo ni Tsh 5,597,000,000. Aidha Serikali ya SMZ inachangia Tsh 600,000,000

Shughuli za msingi za mradi kupitia mradi huu ni pamoja na Ujenzi wa viwanja viwili vya mpira wa miguu ambavyo vitakuwa na uwezo wa kuchukuwa watazamaji 900 na 1200, ujenzi wa jengo la michezo ya ndani (Indoors games) kwa jaili ya mpira wa meza -Table Tennis, majengo kwa ajili ya ofisi, kiwanja chenye uwezo wa kucheza michezo mitatu (Volley ball basketball na netball), sehemu ya mazoezi ya viungo n kuinua vitu vizito, na ujenzi wa Ukuta wa uwanja(uzio)

Kimsingi, Kamati inaipongeza Serikali ya China kwa msaada wao ambao bila shaka utasaidia juhudi za Serikali za kukuza sekta ya Michezo hapa visiwani. Aidha, Kamati inasisitiza sana suala la kuujengea uwanja mazingira ambayo yatauwezesha kudumu katika hadhi yake kwa muda mrefu zaidi, kwa kuuwekea bajeti ya matengenezo yaani "maintenance" pamoja na kuwekewa usimamizi imara wakati utakapoanza kutumika, Kamati inasisitiza masuala haya hasa kwa kuzingatia kwamba imekuwa ni sehemu ya changamoto kubwa kwa miradi mingi ya Serikali inayoanzishwa.

### CHANGAMOTO ZA MRADI

1. Kamati imearifiwa Uwanja hauna eneo la "Parking"
2. Tatizo la kukimbia wafanyakazi wanaofanya kazi katika mradi kutokana na kudai walipwe mara mbili kwa mwezi. Hii ni kutokana na madai kamba, kiwango cha fedha wanacholipwa ni kidogo, ambapo baadhi yao wameamua kuacha kazi.
3. Kamati ilipotembelea Mradi ilibaini wafanyakazi wanafanya kazi bila vifaa vya usalama.

### MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Kwa kuwa sehemu kubwa ya mradi huu ni msaada, na kwa kuwa vibarua wanaofanya kazi hawalipwi viwango vipya vya mishahara vilivyotangazwa na Serikali, Kamati inaishauri Wizara iongeze Bajeti yake katika Mradi huo ilikufidia sehemu ya malipo kwa vibarua hao kwa lengo la kuwawezesha kulipwa kwa mujibu wa viwango vilivyotangwazwa na Serikali.

2. Ili Mradi uweze kuwa endelevu na kupata fedha za kujiendesha hususan katika huduma nyeti kama vyooni. Kamati inashauri sehemu ya vyoo iendeshwe kibishara kwa kutoza ada ndogo kwa watumiaji wa huduma hiyo.

3. Wizara ifanye uchambuzi wa kina mapema ili kujua furasa za kibiashara na uchumi zinazoweza kuibuka katika maeneo ya nje ya uwanja, ili kuja na mpango madhubuti pamoja na kujitayarisha kuhusu shughuli zinazoweza kufanyika wakati uwanja utakapaoanza kutumika.

4. Kamati inashauri Ujenzi wa Mradi uzingatie kutenga sehemu maalum kwa ajili ya huduma za chakula "Cafeteria" ili kuwahudumia watumiaji wa uwanja hususan wanafunzi.

5. Kiwanja kiwekewe Genereta ya akiba "Backup Generator" kwa ajili ya Shughuli za usiku iwapo umeme utakatika.

## SEHEMU YA TATU

## MAONI YA JUMLA YA KAMATI

1. Wizara ya fedha ifanye utafiti wa kina kuhusu uhalisia wa malengo ya ukusanyaji mapato yanayowekwa na taasisi za Serikali kama yanaendana na uhalisia wa uwezo wao wa kukusanya.

2. Serikali itilie mkazo katika kuongeza mapato mengineyo (mapato yasiyotokana na kodi) "Non Tax Revenue" badala ya kujikita kuongeza kodi ambazo humlazimisha mwananchi kulipia moja kwa moja na hatimae kuleta athari kwa mwananchi wa kipato cha chini. Aidha Serikali iongeze ubunifu na usimamizi umadhubuti katika kukusanya mapato, kwa kuwa Kamati imebaini bado kuna baadhi ya wafanyabiashara hawalipii kodi.

3. Kwa kuwa eneo la uwekezaji micheweni bado halijaendelezwa, Kamati inaishauri Serikali kufikiria uwezekano wa kukaribisha wawekezaji ambao watakua tayari kuwekeza viwanda vya kuunganisha bidhaa (Assembling Plants) kwa bidhaa mbali mbali, na hatimae bidhaa hizo kuweza kuuzika katika soko la Afrika Mashariki na kati.

4. Kumekuwa na mashaka juu ya utekelezaji wa mikataba ya kimataifa kwa Serikali ya SMZ kutokana na baadhi ya tozo ambazo zinatozwa na taasisi za Serikali huenda moja kwa moja Serikalini katika mfuko wa hazina kama mapato mfano; tozo za uwanja wa ndege "Safety Fee" pamoja" na "Airport Tax" ambazo zote, kwa mujibu wa mikataba ya kimataifa zinatakiwa zibakie katika mamlaka husika ili kuimarisha huduma za viwanja vya ndege.

5. Katika kukuza ufanisi katika masuala ya kodi, Kamati imebaini umuhimu wa ZRB kuanzisha uwakala kwa kutumia mabenki, makampuni ya simu pamoja na aina yoyote ya mfumo wa kisasa, ili kurahisisha ulipaji wa kodi. Aidha, kutokana na kukua kwa uchumi katika maeneo ya fukwe, Serikali izingatie kuazisha matawi ya ZRB katika miji ambayo inakuwa ili kuwarahisishia wananchi kulipa kodi katika maeneo yao.

6. Kamati inaishauri Serikali kupunguza tatizo la magendo hususani kwa mafuta na bidhaa nyengine zinazofanyika katika visiwa vya Unguja na Pemba. Kuendelea bishara hizo kunaikosesha Serikali mapato. Aidha, Kamati inashauri kutaifisha mali na kuyatangaza majina ya wanaofanya biashara ya magendo (shame list) katika vyombo vya habari, ili jamii iwatambue.
7. Ili kukuza ufanisi wa kiutendaji, Kamati inaishauri Bodi ya Mapato Zanzibar-ZRB kushiriki katika mafunzo, maonyesho na Makongamano ya kimataifa na kikanda kwa kushirikiana na TRA. Katika kulitekeleza suala hilo, Kamati inashauri ZRB wapeleke maombi yao rasmi katika Ofisi ya Waziri wa Jamhuri ya Muungano inayoratibu masula ya Muungano pamoja na Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais Zanzibar.

8. Kamati imebaini kwamba kuna utofauti wa kulipa kodi kwa wafanyabiashara wa mahoteli ambapo baadhi wanalipa VAT na wengine wanalipa "Hotel Levy" ambayo ni asilimia 18. Kwa mujibu wa Sheria ya "Hotel Levy" ya mwaka 1995 ili mfanyabiashara asajiliwe kwenye VAT anatakiwa atimize sharti la kuuza chumba kwa mgeni mmoja kwa kiwango kisichopungua dola 100. Sheria hii inagongana na Sheria ya VAT ya mwaka 1998, inayomtaka kila mfanya biashara ambaye mauzo yake yametimia milioni 30 asajilwe kwenye VAT. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kuangalia upya Sheria zinazohusiana na kodi ili ziendane na mazingira ya biashara husika.

9. Kamati inaishauri Serikali itenge fedha za kutosha katika kuutangaza utalii hasa kwa kuzingatia kwamba sekta ya utalii ina mchango mkubwa katika uchumi wa nchi.

10. Kamati inaishauri Serikali ifanye mapitio ya Sera ya Ushirikiao Baina ya Serikali na Sekta Binafsi (Public Private Pertneship –PPP) pamoja na Sheria namba 8 ya mwaka 2015, inayoiongoza Sera hiyo, kwa kuwa utekelezaji wake unaonekana kuwa mgumu kutokana na

masharti yaliyomo katika Sheria hiyo, ikiwa ni pamoja na kutangaza wazo la biashara la muekezaji kwa ajili ya zabuni.

11. Ili kuwa na ushiriki mpana wa Bajeti kwa wadau na wananchi kwa ujumla, Kamati inaishauri Serikali kuwashirikisha wadau mbali mbali wa Bajeti tokea katika hatua za awali za maandalizi ya bajeti hiyo ili mawazo yao yaweze kuzingatiwa katika bajeti.

**12.** Kamati inashauri Serikali iweke mkakati wa kujenga masoko ya kisasa katika mikoa ambayo biashara ya utalii imeshamiri, ili wafanyabiashara wadogo wadogo waweze kuunganisha nguvu zao kwa kutumia masoko hayo ikiwa kama ni kianzio au chombo cha mwanzo cha kuweza kutambulika rasmi na wenye mahoteli. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuzidi kuwashawishi wamiliki wa mahoteli na makampuni mengine kuzidi kutumia huduma za wazawa katika kutekeleza majukumu yao ya kibiashara.

13. Ili kudhibiti udanganyifu katika mapato ya utalii, Kamati inashauri Wafanyabishara wa Mahoteli kueka wazi huduma zao watakazozitoa kabla ya kupewa leseni ili iwe rahisi kuwadhibiti katika huduma wanazozitoa na kufanya ufuatiliaji. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuzifanyia mapitio takwimu za mahoteli zinazohusiana na usafiri na malazi na madaraja yake kila baada ya miezi mitatu ili kuwa na takwimu sahihi.

**14.** Pamoja na ukweli kwamba makampuni ya mwani yalipunguziwa ushuru ili wazalishaji wa mwani wapate unafuu wa bei hizo, bei ya zao la mwani iliendelea kuporomoka katika visiwa vyetu kutokana na uzalishaji mkubwa unaotumia zana za kisasa katika nchi za Indonesia na Philipine ukilinganisha na zana zinazotumika Zanzibar. Ili kukabiliana na tatizo hilo, Kamati inaishauri Serikali kupanga mikakati madhubuti ya kuinua zao hilo ikiwa ni pamoja na kupeleka wataalamu kujifunza namna ya kusarifu mwani kwa kutengenezea bidhaa mbali mbali.

## SHEHEMU YA NNE

## HITIMISHO

Kamati inapenda kutoa shukurani za dhati kwa taasisi zote za Serikali zilizo shirikiana nayo wakati wa kutekeleza Majukumu yake pamoja na wadau wote walioalikwa na kufika mbele ya Kamati, kwani michango na maoni yao imekuwa ni msaada muhimu kwa Kamati katika kutekeleza majukumu yake ya kuisimamia na kuishauri Serikali. Kamati inasisitiza Serikali kuhakikisha inazingatia Sheria na taratibu zilizowekwa katika kusimamia raslimali za taifa ili kwa pamoja vyombo hivi viweze kuwatumikia vyema wananchi.

**KIAMBATANISHO NO. 1**

## MFUKO WA HIFADHI YA JAMII(ZSSF)

## KITUO CHA BIASHARA MWANAKWEREKWE, MAPATO NA MATUMZI HADI DISEMBA 2018

| MWAKA | MAPATO | MATUMZI |
|---|---:|---:|
| 2009-2010 | 25,896,960 | 6,362,300 |
| 2010-2011 | 155,448,379 | 36,987,200 |
| 2011-2012 | 58,121,000 | 38,173,800 |
| 2012-2013 | 165,454,800 | 39,360,400 |
| 2013 2014 | 104,087,000 | 42,649,436 |
| 2014-2015 | 183,018,000 | 44,027,060 |
| 2015-2016 | 71,630,650 | 51,959,100 |
| 2016-2017 | 138,663,000 | 38,095,836 |
| 2017-2018 | 97,108,000 | 13,526,253 |
| **JUMLA** | **999,427,789** | **311,141,385** |

## KIWANJA CHA WATOTO CHA UHURU KARIAKOO UNGUJA , MAPATO NA MATUMZI HADI DISEMBA 2018

| MWAKA | MAPATO | MATUMZI |
|---|---:|---:|
| 2014-2015 | 656,991,500 | 197,533,175 |
| 2015-2016 | 843,149,000 | 340,709,349 |
| 2016-2017 | 1,191,973,100 | 348,421,260 |
| 2017-2018 | 494,924,000 | 236,141,225 |
| **JUMLA** | **3,187,037,600** | **1,122,805,009** |

## KWANJA CHA KUFURAHISHIA WATOTO CHA TIBIRINZI PEMBA, MAPATO NA MATUMZI HADI DISEMBA 2018

| MWAKA | MAPATO | MATUMZI |
|---|---:|---:|
| 2015-2016 | 157,223,500 | 49,238,664 |
| 2016-2017 | 274,656,500 | 78,558,722 |
| 2017-2018 | 128,230,300 | 57,678,977 |
| **JUMLA** | **560,110,300** | **185,476,363** |

## MNARA A KUMBUKUMBU YA MIAKA 50 YA MAPINDUZI NA BUSTANI YA MCHENZANI MAPATO NA MATUMZI HADI DISEMBA 2018

| MWAKA | MAPATO | MATUMZI |
|---|---:|---:|
| 2015-2016 | 30,029,500 | 20,120,206 |
| 2016-2017 | 40,545,000 | 58,253,703 |
| 2017-2018 | 22,707,000 | 177,018,991 |
| JUMLA | **93,281,500** | **255,392,900** |

**MAPATO YA JENGO LA HOTELI NA OFISI TIBIRINZI**

| MWAKA | MAPATO |
|---|---|
| 2004 | 20,160,000 |
| 2005 | 20,160,000 |
| 2006 | 20,160,000 |
| 2007 | 90,000,000 |
| 2008 | 114,660,000 |
| 2009 | 51,660,000 |
| 2010 | 83,160,000 |
| 2011 | 87,660,000 |
| 2012 | 53,660,000 |
| 2013 | 591,265,901 |
| 2014 | 4,008,704 |
| 2015 | 88,800,000 |
| 2016 | 33,043,000 |
| 2017 | 61,800,000 |
| | **1,312,430,197** |

*Chanzo: Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ZSSF*

***Zingatio*:** Matumizi ya ya Jengo la Hoteli na Ofisi za Tibirinzi kwa kiwango kikubwa yanafanywa na Hoteli zinazokodishwa

**KIAMBATANISHO NO.2**

## SHIRIKA LA BASHARA LA TAIFA (ZSTC)

## MAPATO NA GHARAMA ZA KIWANDA CHA MAKONYO KWA KIPINDI CHA MIAKA MITANO

### TARAKIMU ZOTE KWA ‘000’

| | **2012/2013** | **2013/2014** | **2014/2015** | **2015/2016** | **2016/2017** |
|---|---|---|---|---|---|
| MAPATO YA KIWANDA | 1,037,944.40 | 103,000.00 | 37,166.84 | 767,954.58 | 2,040,800.00 |
| MATUMIZI YA KIWANDA | 1,405,735.75 | 453,000.00 | 629,292.65 | 821,146.81 | 2,055,300.00 |
| HASARA | **-367,791.35** | **-350,000.00** | **-592,125.81** | **-53,192.23** | **-14,500.00** |

*Chanzo: Kiwanda cha Makonyo*

**KIAMBATANISHO NO. 3**

**MAKISIO YA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA MWAKA 2017-2018 HOSPITALI YA ABDALLA MZEE**

| | **KILICHOOMBWA** | **KILICHOPATIKANA** | **MAPUNGUFU** |
|---|---|---|---|
| MAKISIO ROBO YA KWANZA JULAI-SEPTEMBA 2017 | 101,550,000 | 70,000,000 | 31,550,000 |
| MAKISIO ROBO YA PILI OKTOBA-DISEMBA 2017 | 76,900,000 | 50,824,228 | 26,075,772 |
| MAKISIO ROBO YA TATU JANUARI-MACHI 2018 | 94,650,000 | 0 | 0 |
| MAKISIOROBO YA NNE APRIL-JUNI 2018 | 76,900,000 | 0 | 0 |
| **JUMLA KUU** | **350,000,000** | **120,824,228** | **57,625,772** |

*Chanzo: Hospitali ya Abdalla Mzee*

**KIAMBATANISHO . 4**

**WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI**

**MAKISIO YA UKARABATI WA SKULI YA MADUNGU**

| S/N | DESCRPTION | QTY | UNIT | RATE | AMOUNT |
|---|---|---|---|---|---|
| | **SUMMARY** | | | | |
| | **ELEMENT # 1: ROOF** | | | | 122,958,000 |
| | **ELEMENT # 2: CELING** | | | | 28,451,500 |
| | **ELEMEN # 3: WALL, FNISHING AND DECORATON** | | | | 39,772,500 |
| | **ELEMENT # 4: PRILIMANARIES** | | | | 25,000,000 |
| | **Sub total 1** | | | | **216,182,000** |
| | *5% contingence* | | | | 10,809,100 |
| | Sub total 2 | | | | **226,991,100** |
| | *18% VAT* | | | | 40,858,398 |
| | **TOTAL COST** | | | | **TZS 267,849,498** |

*Chanzo: Wizara ya Elimi na Mafunzo ya Amali Afisi ya Pemba*

**KIAMBATANISHO NO.5**

**MAMLAKA YA UWEKEZAJ NA UKUZAJI VTEGA UCHUMI (ZIPA)**
**MIRADI INAYOTEKELEZWA (EXISTING PROJECTS)**

| NAM. | JINA LA MRADI | AINA YA MRADI | GHARAMA ZA MRADI | ENEO ULIOPO MRADI | NCHI WANAYOTOKA WAWEKEZAJI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | ZANEA SEA WEEDS | MWANI | 6,000,000 | PAJE | DENMARK NA ZANZIBAR |
| 2 | SEA WEED AGRO | MWAN/KIWANDA | 140,000 | PAJE | TANZANIA BARA |
| 3 | BIRR SEAWEED | MWANI | 220,000 | WINGWI | SWEEDEN |
| 4 | GIM SEA LTD | MWANI | 510,000 | MSUKA | SPAIN |
| 5 | C. WEED CORPORATON | MWANI | 117,000 | KIUYU | TANZANIA BARA |
| 6 | TRITON | KIWANDA/SAMAKI | 500,000 | MARUHUBU | GREECE NA TANZANIA BARA |
| 7 | FISH & FISH CO. LTD | KIWANDA | 610,000 | KIWENGWA | ITALY |

**MIRADI AMBAYO HAIJAPATA ARDHI NA VIBALI VYENGINE (APPROVED PROJECTS)**

| NAM. | JINA LA MRADI | AINA YA MRADI | GHARAMA ZA MRADI(USD) | NCHI WANAYOTOKA WAWEKEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | SHORELINE | BOTI | 30,000,000 | TANZANIA BARA |
| 2 | HONG DONG | UVUVI BAHARI KUU | 100,000,000 | CHINA |
| 3 | DEEP SEA FISHING GROUP | UVUVI BAHARI KUU | 10,000,000 | CHINA |
| 4 | CTZ | UVUVI BAHARI KUU | 50,000,000 | CHINA |
| 5 | ZANZIBAR S/WEED CENTER | MWANI | 180,000 | TANZANIA BARA |
| 6 | SHRIMP AQUA CULTURE DEVELOPMENT | KIWANDA/KAMBA(SAMAKI) | 20,000,000 | - |
| 7 | FISHING IN THE TERITIRIAL SEA | KIWANDA | 845,000 | TANZANIA BARA |
| 8 | FUJIAN | UVUVI BAHARI KUU | 150,000,000 | CHINA |

**MIRADI AMBAYO HAIJATEKELEZWA (DORMANT PROJECTS)**

| NAM. | JINA LA MRADI | AINA YA MRADI | GHARAMA ZA MRADI(USD) | ENEO ULIOPO MRADI | NCHI WANAYOTOKA WAWEKEZAJI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | PEMBA SEA FOOD(MILIKI) | KIWANDA | 118,000 | PEMBA | - |
| 2 | ZANZIBAR MARINE SEA WEED | MWANI | 50,000 | M/KWEREKWE | - |
| 3 | FISHING INVESTMENT COMPANY | KIWANDA | 2,000,000 | - | - |